# Nipashe

Jumanne Oktoba 20, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580373

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710





UKURASA 11

**MEMBE:** Chagueni mnayeona anafaa



UKURASA 3

**WAWILI** wauawa kwa tuhuma za ujambazi

UKURASA 8

# Pasipoti na leseni ruksa kupigia kura

UKURASA 2



Mgombea urais wa CCM, Dk. John Magufuli, akiwasili kuhutubia mkutano wa kampeni mjini Bagamoyo, mkoa wa Pwani, jana. **PICHA: UKULU**

# JPM aahidi nyongeza ya mishahara

UKURASA 2



Mgombea urais kwa tiketi ya CHADEMA, Tundu Lissu, akihutubia wananchi katika viwanja vya Mnadani, Jimbo la Karatu, mkoani Manyara. **PICHA MPIGA PICHA WETU.**

## BADO SIKU 8



## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### WANUSURIKA KIFO KWA KULA CHAKULA CHENYE SUMU

WATU 152 wakiwamo watoto 79 wamenusurika kufa baada ya kula ...

UKURASA WA 5

### WALIOKUFA KWA MVUA WAFIKA 13

WAKATI Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kesho ukitarajiwa kutoa utabiri mwingine ...

UKURASA WA 8

### UNYANG'ANYI KWA SILAHA WAWAPELEKA JELA MIAKA 30

MAHAKAMA ya Wilaya ya Tarime mkoani Mara, imewahukumu...

## Lissu azuiwa mikutano Arusha

UKURASA 3

**MICHEZO** KAZE AYAONA MABAO YA YACOUBA, SARPONG UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

# Pasipoti, leseni ruksa kutumika kupiga kura

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

ZIKIWA zimesalia siku nane kuelekea Oktoba 28, siku ya kupiga kura, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imetoa nafuu kwa wapigakura, kwa kutoa fursa kwa mpigakura aliyepoteza kadi yake kupiga kura kwa masharti kadhaa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Tume hiyo kupitia mitandao yake ya kijamii, mpigakura huyo ataruhusiwa kutumia kitambulisho mbadala kama vile Kitambulisho cha Taifa, hati ya kusafiria au leseni ya udereva.

Hata hivyo, NEC inasisitiza mpigakura huyo ataruhusiwa akiwa kwenye kituo alichojiandikishia tu na majina yake yafanane na yale yaliyopo kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura.

Agosti mwaka huu akizungumza na vyama vya siasa jijini Dar es salaam, Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mstaafu, Semistocles Kaijage, alisema wapigakura milioni 29,188,347 wanatarajiwa kupiga kura Oktoba 28.

Alisema katika uchaguzi huo kutakuwa na vituo 80,155 vya kupigia kura na watachagua Rais, wabunge 390 na madiwani 5,350.

Kampeni za uchaguzi huo zilianza Agosti 29 na zinatarajiwa kuhitimishwa Oktoba 27, ambapo kila mgombea kwasasa anafanya ushawishi wa mwisho na kukamilisha ratiba ya kampeni.

Licha ya vyama 15 kusimamisha wagombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini wagombea wa vyama viwili Chama cha Mapinduzi(CCM), Dk.John Magufuli na Tundu Lissu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA) ndio wameonekana kampeni zao kutikisa.

Wagombea wa vyama vingine wanaofuata ni Prof. Ibrahim Lipumba wa Chama cha Wananchi (CUF) na Queen Sendiga wa Chama cha ADC ambao wameonekana wakizunguka mikoa mbalimbali nchini.

Ratiba ya kampeni ya wagombea urais, toleo la sita iliyotolewa na NEC, hivi karibuni kuanzia Oktoba 17 hadi 27, imeonesha mikoa ambayo vyama hivyo vitahitimisha kampeni zake huku baadhi vikionesha kufunga kwenye mikoa iliyozindulia.

Katika ratiba hiyo, Dk. Magufuli na Lissu wanaonekana kuelekeza kishindo cha kampeni zao Kanda ya Kaskazini na Kati.

Dk. Magufuli jana alianza awamu yake ya mwisho ya kampeni kuanzia Mkoa wa Pwani kuelekea Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara na atahitimisha kampeni zake Mkoa wa Dodoma ambao alizindulia.

Kwa upande wa Lissu, ratiba inaonyesha jana alifanya mikutano sita kwenye mikoa ya Manyara, Arusha na Kilimanjaro.

Pia ataendelea leo na kampeni Mkoa wa Tanga huku siku zinazofuata atafanya Kusini Pemba, Mjini Magharibi, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Shinyanga, Dodoma, Singida na atahitimisha jijini Dar es salaam ambako ndiko alikozindulia.Ratiba hiyo inaonyesha vyama vya ADC, CUF, CHAUMMA na UMD vitafunga kampeni zake jijini Dar es salam huku AAFP na DP vikihitimisha mkoa wa Songwe.

Vyama vingine maeneo vinapohitimisha kampeni zao yapo kwenye mabano, ACT-Wazalendo (Lindi), ADA TADEA (Simiyu), Demokrasia Makini (Iringa), NCCR-Mageuzi (Mara), NRA (Kigoma), SAU(Mara) na UPDP (Mbeya).



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji (katikati), akikata utepe kuashiria ufunguzi wa Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL) ambayo imefunguliwa tena baada ya kupata uwekezaji wa mtaji wa Sh. Bilioni 7 kutoka Benki ya CRDB. Wa kwanza kushoto ni Naibu Gavana wa Benki Kuu, Dk. Bernard Kibese, akifuatiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay. Wa kwanza kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya KCBL, Dk. Gervas Machimu

# Mbaroni tuhuma kuchana picha mgombea urais CCM

**Na Christina Haule, MOROGORO**

POLISI mkoani hapa inamshikilia Isihaka Exavery (20), mkazi wa Mkundi Manispaa ya Morogoro kwa tuhuma za kuchana picha za mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) na mgombea udiwani wa kata hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 15, majira ya saa tano asubuhi, Mtaa wa Mlimani, mkoani hapa.

Kamanda Mutafungwa alisema kijana hiyo alichana picha za mgombea urais, John Magufuli na mgombea udiwani wa kata hiyo, Seif Chomoka na kukimbia.

Alisema baada ya kupata taarifa hiyo askari polisi walifika eneo la tukio na kufanya msako kwa kushirikiana na wananchi ambao walishuhudia tukio hilo na kufanikiwa kumkamata mtuhumiwa pamoja na picha alizochana.

Kamanda alisema mtuhumiwa anaendelea kuhojiwa polisi ili afikishwe mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

# JPM aahidi nyongeza mishahara

**Na Gwamaka Alipipi, PWANI**

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, amewaahidi wafanyakazi nchini kwamba katika kipindi cha miaka mitano ijayo ataboresha maslahi yao kwa kuongeza mishahara pamoja na marupurupu.

Amesema hiyo ni kutokana na nchi kufikia katika uchumi wa kati, pamoja na ukusanyaji mzuri wa makusanyo.

Alitoa ahadi hiyo jana wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani, wakati akihutubia maelfu ya wananchi na wanachama wa CCM waliojitokeza katika Uwanja wa Mwanakalenge.

"Tumepanga miaka mitano ijayo kuongeza mishahara pamoja na marupurupu ya wafanyakazi, hii ni kutokana na tayari tumeshajenga uchumi na mapato yameanza kuonekana," alisema Dk. Magufuli.

**AHADI MKOA WA PWANI**

Dk. Magufuli pia aliwaahidi wakazi wa Mkoa wa Pwani kuwaboreshea miundombinu ya barabara, ujenzi wa vituo vya afya, zahanati, miradi ya maji, pamoja na hospitali.

Alisema miaka mitano ijayo serikali itakamilisha miradi ya maji ya Chalinze, Mkuranga, Mlandizi na tatizo la ukosefu wa maji katika Mkoa wa Pwani litakuwa historia.

Kuhusu miundombinu, Dk. Magufuli alisema serikali itajenga barabara kutoka Kisarawe hadi Manerumango (km 44), Bagamoyo-Tanga (km 178), itakayopita kandokando ya bahari, Makofia-Mlandizi-Mkurumbu, Kibaha-Mapinga (km23).

Alisema pia serikali itafanya upanuzi wa barabara kutoka Kibaha-Chalinze (km 78) kwa njia nane, pamoja na ujenzi wa barabara kutoka Utete hadi Nyamwage (km 33.7).

"Tunataka kuirudisha Bagamoyo katika enzi zake, nileteeni wabunge na madiwani wa CCM ili huduma na maendeleo yaje kwa kasi," alisema Dk. Magufuli.

**VIWANDA PWANI**

Kadhalika, Dk. Magufuli alisema, Mkoa wa Pwani umekuwa kinara katika ujenzi wa viwanda na sasa una viwanda 1,236.

Alisema mkoa huo kwa mwaka 2015 ulikuwa na viwanda 395, lakini hadi mwaka 2020 umekuwa na idadi kubwa ya viwanda kuliko mkoa wowote.

"Nawapongeza viongozi wote wa Mkoa wa Pwani kwa kazi nzuri waliyoifanya, kuanzishwa kwa viwanda hivyo kumetoa ajira 200,000, kati ya hizo, 50 ni za moja kwa moja, 150,000 siyo za moja kwa moja, nawapongeza kwa ujenzi wa viwanda hivi," alisema Dk. Magufuli na kuongeza:

"Lakini nawaomba wananchi wa Pwani ongezeni uzalishaji wa matunda, limeni matunda, limeni mananasi ya kutosha, litumieni soko hili kutajirika pamoja na kujenga uchumi wa Pwani," alisema Dk. Magufuli.

**WAVUVI PWANI**

Kadhalika, Dk. Magufuli aliwahakikishia neema wavuvi wa Mkoa wa Pwani, kwa kuwatengenezea mazingira bora yatakayowawezesha kuendesha shughuli zao.

Vilevile alisema serikali iko katika mazungumzo na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD), la kununua meli nane zitakazokuwa zinafanya shughuli ya uvuvi katika bahari kuu.

Alisema kati ya meli hizo, nne zitafanya kazi Tanzania bara na zingine katika visiwa vya Zanzibar.

"Tunawakaribisha wawekezaji waje kuwekeza kwenye sekta ya uvuvi, tunataka Bagamoyo iwe na kiwanda cha kuchakata samaki, tumepanga kuendeleza utalii wa fukwe, meli za kitalii kuzuru nchini, pamoja na utalii wa kihistoria na meli kale ufanyike Bagamoyo," alisema Dk. Magufuli.

**MIRADI ILIYOTEKELEZWA**

Pia, alisema katika kipindi cha miaka mitano, serikali imefanikiwa kukarabati shule kongwe za Mkoa wa Pwani zikiwamo Ruvu, Minaki, Kibaha, Bagamoyo pamoja na Kibiti.

Alisema serikali imekarabati hospitali za wilaya ambazo ni Mafya, Kibiti, Mkuranga, Kisarawe, Kibaha, Chalinze, kupeleka magari ya kubebea wagonjwa 12, pamoja na kuajiri watumishi wa sekta ya afya 896.

Alisema pia serikali imetekeleza mradi wa maji wa Ruvu chini kwa gharama ya Sh. bilioni 183.4, pamoja na Ruvu juu kwa ghamara ya Sh. bilioni 105.5, unaohudumia maeneo ya Mlandizi, Kiluvya, Kibaha na Kisarawe.

Kwa upande wake Rais mstaafu, Jakaya Kikwete, akizungumza katika mkutano huo alisema: "Sioni hofu wala wasiwasi kwa wagombea wa CCM, wala wewe (Dk. Magufuli) kushindwa kwenye uchaguzi, kwa sababu chama katika uongozi wake kimefanya mengi mazuri."

Alimtaka Dk. Magufuli kuendelea kufanya kampeni na kwamba hakuna litakalobadilika. Alisema Tanzania ya leo siyo ile aliyomkabidhi Dk. Magufuli madaraka mwaka 2015.

# Lissu akwama mikutano ya kampeni

**Na Waandishi Wetu**

MGOMBEA Urais wa CHADEMA, Tundu Lissu, amekwaa kisiki katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini, baada ya kushindwa kuendelea na ratiba yake ya mikutano ya kampeni katika majimbo ya Arumeru Magharibu na Mashariki.

Baada ya mkwamo huo, Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Freeman Mbowe, akiwa Wilaya ya Hai akimsubiri Lissu kufanya mikutano katika jimbo lake, alilazimika kutuma helkopta nyingine aliyokuwa nayo kwenda kumchukua mgombea huyo ili kuendelea na mikutano yake.

Lissu alishindwa kuhutubia jana katika majimbo hayo yaliyopo mkoa wa Arusha, baada ya helkopta anayoitumia kufanya mikutano ya lala salama, kudaiwa kukosa kibali cha kutua kwenye maeneo hayo.

Jana, Lissu alipaswa kuanza kuhutubia katika Jimbo la Arumeru Magharibi jana asubuhi, lakini baada ya muda mfupi, mgombea Ubunge wa chama hicho, Gipson Ole Meseyeki, alisema Lissu alipotua Uwanja wa Ndege wa Arusha ulioko Kisongo kwa ajili ya kuongeza mafuta, alizuiliwa kwenda kutua na helkopta kwenye uwanja wa mpira wa Shule ya Sekondari Mringa.

Uwanja huo wa Shule ya Mringa ambao ulikuwa ufanyike mkutano huo uko karibu na Uwanja wa Ndege wa Arusha.

Kwa mujibu wa Ole Meseyeki, Lissu, baada ya kukwama kuendelea na kampeni katika eneo hilo aliwasiliana na Mbowe na kumjulisha kilichotokea.

"Kwa kuwa helkopta ya Mwenyekiti wetu wa chama ilikuwa ina kibali cha kutua kwenye uwanja huo wa Kisongo ilitumwa kuja kumchukua Lissu, kwenda kuendelea na mikutano mingine katika majimbo ya Hai na Moshi Mjini mkoani Kilimanjaro," alieleza Gipson.

Aliweleza wananchi na makada wa CHADEMA kuwa: "Mgombea wetu wa Urais akishamaliza mkutano katika Jimbo la Hai, utaratibu wa kupata kibali utakuwa umekamilika na baadae tutaendelea na mikutano yetu tuliyoipanga kuifanya kwa mujibu wa ratiba."

"Ninaomba wananchi mrudi baadae hapa kumsikiliza mgombea wetu wa Urais ana mambo mengi na mazuri ya kuwaeleza kuelekea uchaguzi mkuu oktoba 28, mwaka huu.'

Kwa mujibu wa ratiba, Lissu alikuwa afanye mikutano yake ya kampeni jana katika majimbo ya Monduli, Arumeru Magharibu, Arumeru Mashariki (Arusha) na majimbo ya Hai na Moshi Mjini, mkoani Kilimanjaro.

Katibu wa CHADEMA Jimbo la Arumeru Mashariki, Penzila Pallangyo, alisema katika jimbo hilo Lissu alikuwa ashuke kwa helkopta katika Uwanja wa Shule ya Msingi Leganga iliyopo Usa River, Wilaya ya Arumeru.

Pallangyo alisema Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arumeru, alimpigia simu na kumtaka atafute eneo lingine kwa ajli ya mkutano huo, jambo ambalo alilikataa.

"Sisi tumeamua kufanya mkutano pale pale, kwa kuwa tulipoandika ratiba ya kampeni na kupeleka NEC (kwa msimamizi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi) tulikubaliwa. Sasa wakati wanakubali, hawakujua kama eneo hili lina shule?" alisema Pallangyo.

Katika ufafanuzi wake kuhusu ratiba hiyo, Pallangyo alisema licha ya kuandika barua Oktoba 18, mwaka huu, kwa msimamizi huyo wa uchaguzi, walijibiwa kesho yake Oktoba 19, (jana) kwamba hawaruhusiwi kutumia uwanja huo kwa mkutano.

***Imeandikwa na Allan Isack na Daniel Sabuni (Arusha), Godfrey Mushi (Moshi)**

# Membe awaachia wapigakura waamue

**Na Waandishi wetu**



Mgombea urais wa Chama Cha ACT Wazalendo, Bernard Membe, akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari Dar es Salaam, jana kuhusu mwenendo wa kuelekea uchaguzi mkuu utakaofanyika mwezi huu nchini kote. **PICHA:JUMANNE JUMA**

MGOMBEA urais kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Bernard Membe, amesema wapiga kura wana uhuru wa kumchagua yeye au mgombea kwa tiketi ya Chama Cha Demokrasia na Mandeeo (CHADEMA), Tundu Lissu.

Membe ambaye alikuwa kimya kwa muda mrefu amesema ni lazima Tume ya Uchaguzi Tanzania (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), zihakikishe uchaguzi unakuwa huru na haki kuepusha taifa kuingia katika vurugu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Membe ambaye hajaonekana katika majukwaa ya kampeni tangu arejee nchini kutokea Dubai mwanzoni mwa mwezi uliopita, alisema wapiga kura wako huru kuamua na kikubwa ni maendeleo ya watu.

Alisema Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zitto Kabwe, na Mwenyekiti wa chama hicho, Maalim Seif Shariff Hamad, waliotangaza hadharani kumuunga mkono Tundu Lissu wanao uhuru wa kufanya hivyo na hilo kwake siyo tatizo.

"Wapo watu ndani ya CCM hawatampigia kura Magufuli, wapo watu ndani ya CHADEMA hawatampigia kura Tundu Lissu na wapo watu ndani ya ACT-Wazalendo hawatampigia kura Membe, ni haki yao wawili wameshasema, lakini wanaweza kubadili gia angani kura ni siri," alisema Membe.

"Sisi ni wamoja, hatuna mgawanyiko wowote waliosema ni 'individuals' (binafsi) na tumeyamaliza Chama cha ACT-Wazalendo kina mgombea anaitwa Bernard Membe chama kile kama vyama vingine kimeorodheshwa kwenye fomu ya wagombea urais 15 nipo namba 9 pale," aliongeza Membe.

Vile vile, aliitaka NEC kutenda haki kwa kutangaza matokeo halali ya uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu, ili kuepusha kile alichokiita fujo baada ya uchaguzi.

Kwa mujibu wa Membe, utafiti alioufanya yeye na wenzake kuna dalili za kutokea matatizo katika nchi na kusema kuwa dawa pekee ni kutenda haki.

"Moja kati ya haki inayotakiwa ni ile ya kukubali matokeo na kumtangaza mshindi hata kama wewe umeshindwa na unajiona una pembe sita kubali matokeo," alisema.

Katika suala la kuepusha vurugu, Membe amewataka viongozi wa dini ambao baadhi yao tayari wamejitokeza hadharani kuwaunga mkono baadhi ya wagombea, kuacha mara moja kufanya hivyo, ili kuepusha nchi kuingia katika mgogoro wa kidini jambo ambalo amesema ni la hatari iwapo litaendelea.

Kuhusu upigaji kura ya mapema Zanzibar, alishauri iondolewe na ibakize siku moja pekee ya kufanyika uchaguzi, tofauti na ilivyo sasa kwa kuwekwa siku mbili za kupiga kura ambazo ni Oktoba 27 na Oktoba 28.

Alisema kwa uzoefu wake katika kusimamia uchaguzi barani Afrika katika nchi 19 kama mwangalizi wa uchaguzi, kura mbili liliwahi kujitokeza katika baadhi ya nchi na lilileta matatizo.

"Suala la kupiga kura siku mbili linajenga hisia ya tatizo kutokea mimi kama mwanasiasa mbobevu niliyekwenda nchi 19 kusimamia uchaguzi hili linaweza kuwa tatizo kubwa," alisisitiza Membe.

Alipoulizwa juu ya yeye kutokufanya kampeni, alisema chama hicho bado kichanga na hakina uwezo wa kifedha na kwamba wameelekeza nguvu kwa wagombea udiwani na ubunge katika maeneo 100 nchini.

Akizungumzia sera za chama hicho iwapo kitachaguliwa kuingia madarakani Membe, alisema serikali yake itaweka mazingira mazuri kwa wafanyabiashara ili wawe huru na kuahidi kuwashushia kodi ili waweze kupata faida jambo ambalo amedai halifanyiki kwa sasa na hivyo kufanya wafanyabiashara hao kuwa na mazingira magumu.

Kuhusu kilimo alisema akiwa rais bei ya mazao ya wakulima kama kahawa, pamba, mbaazi na korosho itaamuliwa na soko huku serikali ikipewa kodi pekee na kwamba serikali yake kamwe haitaingilia bei za mazao ya wakulima.

Kuhusu ajira, alisema serikali yake itatumia fedha ili sekta binafsi ziweze kunufaika na fedha hizo na hivyo kukua jambo ambalo litawezesha sekta hizo kuwa na uwezo wa kuajiri na kupunguza tatizo la ajira nchini.

Kwa upande wa uhusiano wa kimataifa, Membe alisema serikali yake itaimarisha uhusiano wa kimataifa ili kukuza ushirikiano wa kiuchumi na kibiashara baina ya nchi.

***Imeandikwa na Enock Charles na Frank Maxmillian (TUDARCo).**

# Lipumba aahidi uchumi wa korosho, gesi kusini

**Na Hamisi Nasri, MASASI**

MGOMBEA urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama Cha Wananchi ( CUF), Prof. Ibrahimu Lipumba, amesema akichaguliwa, atahakikisha serikali yake inaongeza thamani ya zao la korosho kwa mikoa ya kusini.

Amesema ataanzisha viwanda vya kusindika mazao na kutengeneza juisi ya mabibo yanayotokana na korosho.

Lipumba aliyasema hayo wilayani Masasi mkoani Mtwara alipokuwa akizungumza na mamia ya wananchi wa wilaya hiyo kwenye mkutano wake wa kampeni.

Alisema mikoa ya kusini ya Mtwara na Lindi imejaliwa kuwa na rasilimali nyingi ambazo kama zikitumika vizuri uchumi wa mikoa hiyo utapanda na kupunguza umasikini unayowakabili wakazi wa mikao hiyo.

Lipumba alisema kuwa iwapo akichaguliwa kuwa rais atahakikisha anaanzisha viwanda vya kutosha vikiwamo vya kutengeza juisi za matunda kwa kutumia malighali ya mazao ikiwemo matunda yanayotokana na mabibo ya mikorosho.

"Nichagueni kwa kunipa kura za kutosha ili nianzishe viwanda vya kusindikiza mazao, hii itainua uchumi wenu katika mikoa ya kusini ikiwamo hapa wilayani Masasi na pia nitaongeza thamani ya zao la korosho ili iwe na bei ya juu," alisema Lipumba.

Alisema wakulima wa korosho katika mikao hiyo wameendelea kuwa masikini licha kulima korosho kwa miaka mingi kutokana na bei inayolipwa kwa wakulima kuwa ndogo.

Alisema bei hizo zimeendelea kumgandamiza mkulima na kuendelea kuwa masikini, lakini kupitia viwanda hivyo iwapo CUF ikipata ridhaa ya kuongoza nchi kitahakikisha inaongeza thamani na uchumi wa kusini unaimarika zaidi.

Kwa mujibu wa Prof. Lipumba, mazao mengine ambayo serikali ya CUF ikiingia madarakani pia itayaongeza thamani ni mbaazi, choroko na ufuta lengo likiwa ni kumuinua mwananchi.

Aidha, Lipumba alisema atatumia rasilimali ya gesi katika kukuza uchumi wa kusini kwani rasilimali hiyo kwa sasa haitumiki vizuri licha ya kuwa muhimu kwa kusini.




Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isaack Kamwele, akizindua kivuko cha Mv.Ukara II iliyowasili katika Kijiji cha Bwisya kisiwa cha Ukara wilayani Ukerewe, kivuko hicho ni mbadala wa Mv.Nyerere iliyozama September 20, mwaka 2018 ambapo watu takribani 227 walipoteza maisha.
**PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# TAKUKURU yaonya pilau kusherehekea ushindi uchaguzi

**Na Joctan Ngelly, GEITA**

MKUU wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoa wa Geita, Leonidas Felix, amepiga marufuku wapigakura kwenda kula pilau kwa watakaoshinda katika uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu na watakaobainika watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Felix alitoa onyo hilo wakati akizungumza na waandishi wa habari jana, na kusema wapigakura kula kwa kiongozi aliyeshinda ni kupokea rushwa ya vyakula, ambayo itawafanya wakose nguvu za kuwahoji shughuli za kuwapelekea maendeleo.

Aidha, alisema kula chakula kwa wagombea waliyoshinda ni kumalizana mkataba kati ya mgombea na mpigakura. Kwa sababu kufanya hivyo kiongozi aliyeshinda hawezi kujishughulisha kuwapelekea maendeleo kwa sababu wamemalizana kwenye pilau.

Felix alisema kwa sasa wapigakura waamishe akili zao za kuwaza kula pilau badala yake wahudhurie kwenye mikutano ili kusikiliza ilani za wagombea waweze kufanya uchaguzi sahihi ifikapo Oktoba 28, mwaka huu.

Aidha, aliwataka wapigakura kutunza vitambulisho vyao vya kupigia kura na wasiruhusu watu wasio wema kuvinunua na watakaobaini wakifanya hivyo watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Alisema wapiga kura watambue dhama ya kura yao ni haki anayohitaji, utulivu anaohitaji, amani anayohitaji na maendeleo anayohitaji katika maeneo yao wanayoishi.

Aidha, aliwataka wapigakura pindi waonapo wagombea na wapambe wao wanaofika majumbani mwao kwa kuwapatia zawadi mbalimbali watoe taarifa katika ofisi za TAKUKURU zilizopo karibu nao.

**Felix alisema kwa sasa wapigakura waamishe akili zao za kuwaza kula pilau badala yake wahudhurie kwenye mikutano ili kusikiliza ilani za wagombea waweze kufanya uchaguzi sahihi ifikapo Oktoba 28, mwaka huu.**

# CHADEMA yataka miradi ya kuondolea watu umaskini

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

MGOMBEA Mwenza wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia CHADEMA, Salum Mwalimu, amesema uwekezaji wa miradi ya maendeleo endelevu ndiyo wenye kusaidia uchumi wa nchi na kuondoa umaskini wa wananchi.

Alisema hayo wakati akihutubia wakazi wa mji wa Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera katika uwanja wa Shule ya Msingi Kashi.

Mwalimu alisema jambo moja la uchumi linaloweza kuzalisha maendeleo ya wananchi kwa ni kutumia rasilimali za gesi zilizopo kwenye mikoa ya Lindi na Mtwara, ambayo ndiyo yenye thamani kubwa dunia.

Alisema kuwa fedha za sekta binafsi ndizo zinaweza kuleta maendeleo ya watu kwa kuwekeza katika kujenga bandari kubwa ya Bagamoyo ambayo italeta fursa kubwa kwa wananchi

"Watu wangeshusha mizigo ya bidhaa na kupeleka mizigo kwenye maeneo mbalimbali kwa kushika bidhaa zao kwenye bandari hizo," alisema Mwalimu.

Alisema usimamizi wa sera za uchumi ambao unaofanywa kwa kipindi hiki, hauangalii mahitaji ya jamii ya watu wa hali ya chini inayotafuta pesa kwa kutegemea uzalishaji mdogo.

Aidha, alisema ukusanyaji wa mapato unaofanywa na serikali kwa sasa kipindi hiki ulitakiwa ufanywe na sekta binafsi, ambayo inaweza kuchangia pato kubwa na kukuza uchumi.

"Sekta za usafirishaji hasa kampuni binafsi ndiyo yangetengeza ujira kwa kugawana na kuongeza uchumi unaokua zaidi," alisema Mwalimu.

Mwalimu alisema kuwa CHADEMA inaamimi kuwa uchumi wa nchi unaweza kukuzwa kupitia gesi na bandari, hivyo kuinufaisha jamii.

"CHADEMA tunataka tuanze na barabara za vijijini kuongeza shughuli kuu za kilimo, ndivyo chama kinavyoamini," alisema.

"Kahawa itauzwa popote unapotaka kama unataka kuwa na tani zako 20 za kahawa lipa kodi, tunaamini kwenye sekta binafsi kwa kutaka maendeleo ya watu." alisema Mwalimu.

# Mgombea urais AAFP aonya wanaoshabikia yasiyo na tija

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA wa urais kupitia Chama cha Wakulima Tanzania (AAFP), Seif Maalim Seif, amesema uchaguzi mkuu wa mwaka huu umeonyesha jinsi Watanzania wasivyo na uelewa na weledi wa maana ya demokrasia ya mfumo wa vyama vingi.

Akizungumza katika mahojiano maalum na gazeti hili jana, alisema katika kipindi cha miongo mitatu ya demokrasia ya vyama vingi kinachoonekana ni ushabiki wa mambo ambayo hayana maslahi na tija kwa taifa.

"Imefikia hatua kila mtu ni mshabiki tu na hatari zaidi ni kwa viongozi wa dini kujiingiza katika siasa na kuvishabikia baadhi ya vyama jambo ambalo siyo zuri kwa usalama wa nchi," alisema.

Seif alisema ni lazima mambo haya yakemewe kwa kuwa demokrasia siyo tu kutofautiana kifikra, lakini ni suala la kuonyesha uzalendo na utaifa kwa nchi.

Alisema wananchi na viongozi wa vyama vya siasa lazima watambue kuwa siasa siyo uhasama, demokrasia ni pamoja na kutaka watu kuishi pamoja kwa amani na upendo.

"Hivi sasa mpira wa miguu umekuwa na ustaarabu kuliko hata demokrasia ya siasa, tunapoelekea katika uchaguzi hata akija nani akaendesha uchaguzi huu mshindi akapatikana bado demokrasia itakuwa haizingatiwi," alisema.

Seif alisema kama Watanzania watampa ridhaa siku 100 za mwanzo kipaumbele chake itakuwa ni kuwaunganisha wananchi bila kujali nani mshindi ili kujenga umoja wa kitaifa.

Aliongeza kuwa hivi sasa Watanzania wamegawanyika kwa milengo tofauti ya kisiasa hali ambayo imejitokeza katika kipindi cha kampeni.

# Wanusurika kifo kwa kula chakula chenye sumu

**Na Pendo Thomas, KIGOMA**

WATU 152 wakiwamo watoto 79 wamenusurika kufa baada ya kula chakula kinachodhaniwa kuwa na sumu katika sherehe ya kuzaliwa watoto wawili.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, James Manyama, alisema tukio hilo limetokea Oktoba 17 majira ya saa mbili asubuhi katika familia ya Tamu Zimbwe, Kijiji cha Kigadye, wilayani Kasulu, mkoani Kigoma, wakati wananchi wakiwa kwenye sherehe.

"Wakiwa wamejumuika walikula chakula aina ya wali maharagwe na kinywaji aina ya mtobe au togwa, lakini baada ya muda hali zao zilianza kuwa mbaya na kuanza kutapika, kuharisha na kuishiwa nguvu hivyo kutoa taarifa polisi," alisema.

Alisema timu ya watalamu wa afya kwa kushirikiana na polisi walifika katika kijiji hicho kutoa huduma ya kwanza na waathirika wa tukio hilo walipelekwa kituo cha afya cha kambi ya wakimbizi ya Nyarugusu kwa matibabu.

Alisema watu 34 wakiwamo watoto 31 na watu wazima watatu hali zao zilikuwa mbaya na kuhamishiwa hospitali ya Wilaya ya Kasulu kwa matibabu zaidi.

Jeshi la Polisi linamshikilia baba wa familia hiyo, Tamu Zimbwe kwa uchunguzi wa tukio hilo.

"Hakuna aliyefariki, lakini tunamshikilia mwenye familia kwa mahojiano zaidi," alisema.

Mganga Mkuu Wilaya ya Kasulu, Robert Rwebangira, alisema waliowapokea wamelazwa Hospitali ya Wilaya ya Kasulu kwa ajili ya matibabu zaidi na afya zao zinaendelea vizuri.

"Chakula, kinywaji na matapishi vimepelekwa katika ofisi ya Mkemia, Mkoa wa Mwanza kwa ajili ya vipimo ili kubaini uhalisia wa tukio hilo," alisema.

# Waliokufa kwa mvua Dar wafika 13

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI Mamlaka ya hali ya Hewa Tanzania (TMA) kesho ukitarajiwa kutoa utabiri mwingine wa mvua kwa mikoa inayopata mvua mara moja kwa mwaka,

Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limesema watu waliokufa kutokana na mafuriko imefikia 13.

Idadi hiyo imefikiwa baada ya mwingine kuopolewa kwenye bonde la Mto Msimbazi hivi karibuni.

Akizungumza na Nipashe jana kwa simu, Kamanda wa Kanda maalum ya Dar es Salaam,

Lazaro Mambosasa, alisema miili hiyo ilishakabidhiwa kwa familia kwa ajili ya mazishi.

"Idadi ya watu waliokufa sasa imefikia 13, kuna mwili umeonekana mto Msimbazi na jeshi la polisi linaendelea kufuatilia kwa karibu kuona

kama kuna athari nyingine au kuonekana kwa miili mingine zaidi, tutatoa taarifa kila kunapotokea au tukibaini kitu," alisema Kamanda

Wakati huo huo, TMA iliieleza Nipashe kuwa leo itatoa utabiri mwingine kwa mikoa inayopata mvua mara moja kwa mwaka.

## CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)

Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) anawatangazia wote walioomba nafasi ya kukitumikia Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kwa nafasi ya katibu wa Wilaya, kuwa usaili utafanyika siku ya Jumatano tarehe 11 Novemba 2020, kuanzia saa mbili asubuhi katika ukumbi wa LAPF Jijini Dodoma.

**MUHIMU**

1. Kila msailiwa aje na kitambulisho cha uanachama.
2. Gharama za usafiri, chakula na malazi zitakuwa juu ya msailiwa.

| NA. | JINA | NA. | JINA |
|---|---|---|---|
| 1. | ABDALA SAKIBU | 2. | JUSTUS RICHARD KAGYA |
| 3. | ABEL SHELIE | 4. | KASSIM ALLY MGUNYA |
| 5. | ACHIENG RUBBY ODAMO | 6. | KERARIYO EMMANUEL |
| 7. | ADAM SEVERINE KYARA | 8. | KERENGO MSAKAMBI TANGAZO |
| 9. | ADRIA CALIST | 10. | KIBIBI ATHUMAN LUKINDO |
| 11. | ADVENTINA ISHOTA | 12. | KIDUMA GOD |
| 13. | AGUSTINO LEHHO SULLE | 14. | KIMBUTE MDEE |
| 15. | AIBORO KESHORI | 16. | KIPANDE MIKIDADI HUSSEIN |
| 17. | ALANI ELIUD | 18. | KISMA EVANCE |
| 19. | ALBINUS P. ZAKARIA | 20. | KOLMAN MRUMA |
| 21. | ALICE CHOAJI | 22. | KULWA MTEBE |
| 23. | ALLEN LAWRENCE CHUKWA | 24. | KUNYARA MSANGYA EDWARD |
| 25. | ALLI FERUZI | 26. | KWIGIZE ALEX BALTHAZAR |
| 27. | ALLY KANUMGUNDA | 28. | LADISLAUS BENEDICT |
| 29. | ALLY RAMADHANI DASARE | 30. | LADISLAUS MKUU |
| 31. | AMIN KIBONA | 32. | LEVINA M. RUGAITIKA |
| 33. | AMOS JUVENARY | 34. | LILIAN COSTANTINE |
| 35. | ANDREA A. KOMBO | 36. | LOTHA LAIZER |
| 37. | ANDREW NGAZU | 38. | LUCAS MWILENGA |
| 39. | ANDREW NYAWENA | 40. | LUCY LONGINO |
| 41. | ANITHA MATFUNGWA | 42. | LUGEMA DODO |
| 43. | ANNA CHAMBUSA | 44. | LUHENDE LUCHANGULA |
| 45. | ANNA ZUMBA | 46. | LUHENDE LYONGOMA |
| 47. | ANNASTAZIA MUNGA'AHO MASSAWE | 48. | MAGERO PAUL MISANA |
| 49. | ARON MNYAMPI ELIUD | 50. | MAGINA EGATA |
| 51. | ASHURA HASSAN MASOLI | 52. | MAGRETH MABULA |
| 53. | ASHURA SONDA | 54 | MAHUVI MAPEMBE |
| 55. | ATHUMANI LIKEYEKEYE | 56. | MALKIA JAMES NYAMANDEGE |
| 57. | BABY TAMBUKO | 58. | MARIA BARNABAS KAZIMOTO |
| 59. | BAHATI KULWA | 60. | MARIAM RASHID |
| 61. | BAHATI MLYUKA | 62 | MARTHA Y. MGINA |
| 63. | BENJAMINI KAHUNGA MAYENGELA | 64. | MARWA KERENGO NYAKOREME |
| 65. | BONIPHACE OTAIGO MARWA | 66. | MARY CHARLES |
| 67. | BULILO MAIRA | 68. | MARY NDERE |
| 69. | BYERA BENOBIRE | 70. | MARY YUVENALY MOSHI |
| 71. | CALVIN ISRAEL MWIHOMENE | 72. | MARYELIZABETH AUGUSTINO |
| 73. | CASSIAN NGORONJE | 74. | MASALU BUDAKA |
| 75. | CHACHA MARO MKWIBE | 76. | MASENA HERMAN VICTOR |
| 77. | CHACHA NYAKIMORI MAGESA | 78. | MASHAURI MAKOE |
| 79. | CHARLES ROBERT TESHA | 80. | MASHINDANO JOHN PILIKANO |
| 81. | CHARLES S. DANIEL | 82. | MASUMA SHABAN |
| 83. | CHESTA STANSLAUS KOMBE | 84. | MATUKU MUGETA |
| 85. | CHIPETA MBARUKU | 86. | MAWAZO MOHAMEDI |
| 87. | CHRISTINA MWISOMBA | 88. | MAWAZO PONIAGA |
| 89. | CHRISTOPHER ESTOMI | 90. | MAXON MABOJE |
| 91. | CHRISTOPHER KABALIMO | 92. | MDAKI JUMA RAJABU |
| 93. | CHRISTOPHER MAKELELE | 94. | MECKSON Y. WIDZENGO |
| 95. | CLETUS MTENGA | 96. | MENSON L.S. MKWAWA |
| 97. | CLOFORD MKWAMA | 98. | MESHACK M. MPENDA |
| 99. | COSMAS NZUNDA | 100. | MGENDI NYABENGE |
| 101. | COSMAS ZENOBIUS NDUNGURU | 102. | MGETA MALIMA CHARLES |
| 103. | CRISTOPHER NYAKERERE | 104. | MKAMA S. BUNYINYIGA |
| 105. | DAMAS HOSTERI | 106. | MOHAMED ALLY MWENDA |
| 107. | DANIEL MAFURU | 108. | MOHAMED ALLY SAAD |
| 109. | DANIEL WENSISLAUS MAJENGA | 110. | MOHAMED O. MBINDE |
| 111. | DAMARI ELIEZA SEMANGO | 112. | MOHAMED SEIF ABDALLAH |
| 113. | DAUD ONESPHORY MINJA | 114. | MOHAMED SULEIMAN LITANGWE |
| 115. | DENIS DIVA WASAGARA | 116. | MONGSON MOHAMED KABEHO |
| 117. | DEODATUS JULIUS MTITU | 118. | MSAFIRI MFINDI |
| 119. | DEUS NKAKIBONA | 120. | MSONGE WILLIAM |
| 121. | DIOCRES M. FELICIAN | 122. | MTARO MZIRAI |
| 123. | DISIOLE MWEGALAWA | 124. | MUKUSIN M. IBRAHIM |
| 125. | DISMAS KATATA MBARAMWEZI | 126. | MUSTAFA SEMVUA |
| 127. | DOMINIC ABIUDI KILONZO | 128. | MWANAHAWA RAMADHANI MGANGA |
| 129. | DOMINICK PELEUS | 130. | NATHANAEL ELIAD |
| 131. | DOSEPH C. NDALAMA | 132. | NEEMA A. LWILA |
| 133. | DOTO MASANJILA | 134. | NEEMA PAUL |
| 135. | DOTTO SULEIMAN | 136. | NELDA TIMANYIKA |
| 137. | DUNIA G. LUVEVA | 138. | NESTORY SELEMAN |
| 139. | ECKRIA JACKSON MAPYA | 140. | NEZIA M. MKAMA |
| 141. | EDINA ELISHA KALAMBO | 142. | NG'HUMBA GEORGE |
| 143. | EDWARD K. EDWARD | 144. | NKANE NKANE ALLY |
| 145. | EDWARD PARTEIYE | 146. | NOELA SHEBBY MLWAFU |
| 147. | ELIAS M. GENGE | 148. | NURU SEIF |
| 149. | ELIEZA CHIMELESA | 150. | NYABUGUMBA GRACE HAMISI |
| 151. | ELINA PALANJO | 152. | OBADIAH Z. BUHOTOLA |
| 153. | ELISANTE BENJAMINI KINDULI | 154. | OMBENI MKAMBA |
| 155. | EMMANUEL HUSEIN | 156. | OMBORI ISACK |
| 157. | EMMANUEL P. JOHN | 158. | ONESPHORY BYABUSHA |
| 159. | EMMANUEL URASSA | 160. | ORESTER REYNER NYENYEMA |
| 161. | ESSAU SIMON KATOSANI | 162. | OSCAR OTIENO MAGORI |
| 163. | ESTER MULUNGU | 164. | OTEA MAKUKUMA JOHN |
| 165. | ESTHER EMMANUEL LYANGA | 166. | PAMPLIUS ABEL |
| 167. | ESTHER LAZAROUS | 168. | PASCHAL REUBEN |
| 169. | EUSTADIUS MKULU FIDELIS | 170. | PAUL ERNEST MWAGO |
| 171. | EVELINE KAALE | 172. | PAUL JOSEPH MSANJILA |
| 173. | EVODIUS HENERICO | 174. | PETER CLEMENT SHEHIZA |
| 175. | EVODIUS POUL KANYANANGIRA | 176. | PETER LUKUMAY |
| 177. | EVON GIDEON MHEWA | 178. | PETRO PAUL WELLA |
| 179. | EZECK MBAZIKAGUO | 180. | PETRO S. BASILI |
| 181. | FAIDA D. POUL | 182. | PHENEHAS DAVID |
| 183. | FAITH KATUNZI | 184. | PHILOMENA M. SOLOMON |
| 185. | FARAJA EMMANUEL MGINA | 186. | PHILOMENA O. SIMION |
| 187. | FEDSON JUSTIN MUHOLI | 188. | PIUS PAUL KILIBA |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 189. | FEITH PATRIC MUNG'ONG'O | 190. | PROSPER MUTUNGI |
| 191. | FIDEA YOHANA MAKUYU | 192. | RAHEL MATINDE |
| 193. | FIDELIS KAKUNDA | 194. | RAINER STEPHEN KAYOMBO |
| 195. | FIKIRI JB MGINA | 196. | RAJABU A. MSUYA |
| 197. | FLOLING RWELA | 198. | RAJABU MTUNZI SALUMU |
| 199. | FORTUNATUS DAMAS KAYAMBA | 200. | RAMADHANI AHMED KARAWA |
| 201. | FRANCIS A. CHAMBO | 202. | RANGE R. MARWA |
| 203. | FRANCIS KISUKILO | 204. | RASHID HASSANI KAJONJO |
| 205. | FRANCIS MAUKAH | 206. | RASHID NASSORO TEBE |
| 207. | FRANK D. LUPEKE | 208. | RASHID NYAKIMWE |
| 209. | FRANK SAIBA MWAKABANJE | 210. | REBECCA CHARLES KIPANGULA |
| 211. | FREDRICK EDWIN FUNGO | 212. | REGAN RIWA |
| 213. | FREDRICK PETER KASUKA | 214. | REHEMA MWANGOKA |
| 215. | FREDY MWIGA | 216. | RELIEF JULIUS MTENGA |
| 217. | GAUDENS ZENO MBANILE | 218. | REUBEN SOTI |
| 219. | GEOFRE MUGISHA | 220. | RHOBIRI ZACHARIA |
| 221. | GEORGE KAHANDA | 222. | RHODA MICHAEL MWINUKA |
| 223. | GEORGE UBUYU | 224. | RIDHIWANI MSUYA |
| 225. | GLORIA SPOTWA | 226. | RIZIKI A. FUNGO |
| 227. | GODFREY MAKOLO | 228. | ROBERT NYAWALA SALALA |
| 229. | GODFREY VENANCE NSILIMWA | 230. | ROSE RWECHUNGULA |
| 231. | GODLISTEN KABARATA | 232. | ROSE SOSPETER |
| 233. | GODLOVE JOSEPH SHILA | 234. | RUGUMBA JOSEPH |
| 235. | GODSON GORDON MWAIBINGILA | 236. | SABATO MNIKO |
| 237. | GOODLUCK SHOO GAMALIEL | 238. | SABINA LIPUKILA |
| 239. | GOSBERT NYAKAYANGO | 240. | SAID RAMADHAN |
| 241. | GOZIBERT B. REVELIAN | 242. | SAIDI JUMA MCHALAGANYA |
| 243. | GRACE MSACKY | 244. | SALMA RIZIKI KIMARO |
| 245. | GRACE T. MAHENGE | 246. | SALUM NGUMBI |
| 247. | HABIBU R. BUNDALA | 248. | SAMSON ELIAS NYABINYILI |
| 249. | HADIJA J. NG'UNGU | 250. | SAMWEL MASSEKE DANIEL |
| 251. | HADIJA MOHAMED HALFANI | 252. | SEBASTIAN EZEKIEL GUNDA |
| 253. | HADIJA MOHAMED MSOFE | 254. | SELEMAN ABDALLAH KARAVINA |
| 255. | HAFSWA MUSSA MNYANDI | 256. | SELEMAN NG'AMBI |
| 257. | HAJI RASHID CHONYA | 258. | SENGONDO ELISANTE SENGONDO |
| 259. | HALIFA SALEHE MFANGA | 260. | SHADRACK MBWILO |
| 261. | HALIMA FLORENTINE MNDEME | 262. | SHARIFA KHATIBU MNGWALI |
| 263. | HAMIS HUSSEIN | 264. | SHARIFA M. NNILEKA |
| 265. | HAMIS JUMA | 266. | SHEKIFU YOHANA |
| 267. | HAMIS MWANDALA | 268. | SHELUKINDO Y. SHEKIFU |
| 269. | HAMZA MARWLE | 270. | SIBORA KISHERI |
| 271. | HAPPINES AVIRET RICHARD | 272. | SIFA LUCAS MBEMBELA |
| 273. | HAPPINES C. BANIKWA | 274. | SILINO A. KALINGA |
| 275. | HAPPYFANIA YABA | 276. | SILVIA KIDIBULE |
| 277. | HARUNA RAMADHANI KAMBI | 278. | SIMON PENDAHERI |
| 279. | HASSANI MURTAZA KONGOI | 280. | SOLANITHA J. MCHUNGUZI |
| 281. | HASSANI SEIF MPWAPWA | 282. | SOPHIA BAKARI |
| 283. | HILDA LYIMO | 284. | SOPHIA DEOGRATIAS KITOBELO |
| 285. | HOLDESIFA NDEMFOO | 286. | SOSPETER MASHOKA |
| 287. | HONESTER PETER MWILENGA | 288. | SOSTENES C. HAULE |
| 289. | HURUMA J. KILINGO | 290. | STELAH JOEL MSUYA |
| 291. | IDRISA SELEMANI | 292. | STEPHANO NADE AKONAAY |
| 293. | IMAKULATA ROMANUS HAULE | 294. | SUBILAGA SNATH MWAMWEZI |
| 295. | INNOCENT MGULISI | 296. | SUDI IDD SUDI |
| 297. | ISACK MWALWAJO | 298. | SUMAYI VERONICA JAMES |
| 299. | ISACK NEWTON MWAIJANDA | 300. | TABITA MABULA KILYABUMU |
| 301. | ISAYA EMMANUEL | 302. | TANO ELIASA |
| 303. | JACKRINE RICHARD | 304. | TATU KINGWALA |
| 305. | JAHA MWENKALA | 306. | TATU OMARI MWOKEACHAO |
| 307. | JAMES KANGARO | 308. | TEDDY KAHWA |
| 309. | JAMES RWEGASIRA NDYANABO | 310. | THADEO BWANA MSOMI |
| 311. | JAMES VITUS MAKUYU | 312. | THOMAS ANTHONY THOMAS |
| 313. | JAMES WAMBURA | 314. | TIBIANUS NJIA PETER |
| 315. | JAMIRA HABIBU YAHAYA | 316. | TUKAHIRWA J. RUNYORO |
| 317. | JANE SHOO | 318. | TUMAINI DANIEL |
| 319. | JEKONIA ELIAB | 320. | TUMWENDAGE JOHN KADUMA |
| 321. | JIMMY JOHN MUNGURU | 322. | TWALIBU OMARY MCHANDO |
| 323. | JOANE ESTON KASAMBALA | 324. | UPENDO P. MWAKALOBO |
| 325. | JOEL BUZUKA | 326. | VAILET MELARY |
| 327. | JOEL MHOJA JUSTINE | 328. | VAILETH D. L. KISHOA |
| 329. | JOHN ANGELIUS KIGONGO | 330. | VENANCE SYLIVESTER |
| 331. | JOHN DOTTO CASSIANO | 332. | VERENA DAVID |
| 333. | JOHN MABEYO | 334. | VESTINA LUBAO |
| 335. | JOHN MUTUGUMONGA | 336. | VICKY MROSSO |
| 337. | JOHNSTON LUMENYERA | 338. | WILLIAM GEORGE KANYONDO |
| 339. | JONAS MHOKA MALYSHAMBA | 340. | YAHAYA MGAZA RAMADHANI |
| 341. | JONAS RODENI | 342. | YARED SELEH YOWAS |
| 343. | JONATHAN ERASTO LOSIOKI | 344. | YAVAN NKUNDWA |
| 345. | JOSEPH BEDA MPUMBE | 346. | YESAYA IBRAHIM |
| 347. | JOSEPH MASOLWA MISALABA | 348. | YOHANA KODI FEO |
| 349. | JOSEPH MHAMIS | 350. | YUDATHADEY NICODEMU SUMAILI |
| 351. | JOSEPH SAIMON KIHWELE | 352. | YUSUPH MUSSA HAMISI |
| 353. | JOYCE JOSEPH MSHANA | 354. | YUSUPH TARIMO |
| 355. | JOYCE KAISHOZI | 356. | ZABIUNA KARIBI NCHIMBI |
| 357. | JOYCE KALEKEZI | 358. | ZEBEDA KHASSIM CHIKOKO |
| 359. | JULIANA LUBUVA | 360. | JUMA SIMON MTUNDI |
| 361. | JUMANNE MSOMBA | | |

Imetolewa na:

Mwl. Deus G. Seif
**KATIBU MKUU – CWT.**
**20/10/2020**

215950402

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# NEC, ZEC zitende haki kwa mawakala wa vyama vyote

ZIMEBAKI siku nane ili Watanzania wafanye uamuzi ndani ya sanduku la kura juu ya nani atawaongoza katika ngazi ya kata kwa ajili ya kuwawakilisha katika Baraza la Madiwani, Jimbo kwa ajili ya kuwawakilisha katika chombo cha kutunga sheria na kuisimamia serikali na rais wa kuiongoza Tanzania kwa miaka mitano ijayo.

Kwa sasa kila mgombea anakimbizana na wakati kuhakikisha anafanya ushawishi wa mwisho kwa wapigakura kumchagua kushinda nafasi anayoomba, huku kilio kikubwa kikiwa ni uchaguzi huru na haki.

Ili kujiridhisha na kinachoendela katika kituo cha uchaguzi ni kuhakikisha kila wakala aliyeteuliwa na chama anapata nafasi sawa kuona, kusaini na kupata nakala ya matokeo ya kituo chake.

Kwa mujibu wa sheria, kila chama hutakiwa kuwa na wakala ambaye anakuwa ndani ya kituo cha kupigia kura, ambaye anakuwa ni jicho la chama husika katika misingi ya uchaguzi kuwa huru na haki, ikiwamo kila chama kujiridhisha kuwa haki imetendeka na hakuna udanganyifu.

Mara kadhaa imejitokeza kuwa mawakala hawakupewa nakala za matokeo na hata kunyimwa kusaini au kutotambulika katika vituo

Kumekuwa na kilio cha muda mrefu kwa vyama vya upinzani mawakala kunyimwa kuingia kituoni kwa sababu mbalimbali, kunyimwa nakala ya matokeo jambo ambalo linakosa uwakilishi unaotakiwa.

Tayari baadhi ya wagombea wameanza kupaza sauti juu ya utaratibu wa kuwapo mawakala vya vyama kwenye vituo, kwamba watapewa barua na Msimamizi wa Uchaguzi wa jimbo au kata ambao ni Mkurugenzi wa Halmashauti au Manispaa na watendaji wa kata.

Wagombea hao wanataka mawakala hao kupewa barua za utambulisho mapema, tofauti na hali ilivyosasa kwamba watazikuta barua kwenye vituo walivyopangiwa.

Hofu inayotajwa ni kuwa huenda mtu apatapagwa kituo "A" lakini kumbe barua yake imepelekwa kituo "B" na hadi anafanikiwa kuipata tayari chama husika hakina jicho ndani ya kituo cha uchaguzi jambo ambalo siyo sahihi.

Pia, wagombea wameomba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kuhakikisha kila wakala anapewa nakala ya matokeo yaliyosainiwa, ikiwa ni namna ya kujiridhisha kilichofanyika ni sahihi.

Katika hili, tunatarajia NEC kutenda haki kwa vyama vyote ili kuondoa lawama ambazo zitazua hisia za upande flani kupendelewa, lakini kukiwa na uwazi pamoja na ushirikishwaji maana yake hakutakuwa na malalamiko.

Pia, vyama vihakikishe vinakuwa na mawakala kila kituo na si kulalamika kwenye majukwaa ya kisiasa, au baada ya uchaguzi.

Ni lazima vyama vitoe elimu kwa mawakala hao juu ya namna ya kufanya kazi hiyo ipasavyo, kufuata taratibu ikiwamo kuhakikisha wanakuwa na nakala kuliko kulalamika bila ushahidi.


Upo ushahidi kuwa nyakati za uchaguzi ndipo taifa hugawanyika vipande vipande kutokana na matendo na kauli za wanasiasa na wafuasi wao, na hali huwa mbaya zaidi kama wenye wajibu wa kusimamia watashindwa kutekeleza wajibu wao kwa kuzingatia sheria.

Ni matarajio yetu kuwa NEC na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) zitatimiza wajibu wao kisheria pasipo kumwonea au kumbeba yoyote, bali kile kitakachoamuliwa na wananchi ndani ya sanduku la kura ndicho kitakacho zungumza.

Kilio cha haki kwa wote ni kikubwa na haitarajiwi haki hiyo kusiginwa kwa namna yoyote bali kufuata misingi ya kidemokrasia katika kupata viongozi kwa miaka mitano.

Haki huinua taifa na siku zote haki ikisimama basi hakuna vurugu au uvunjifu wa amani unaoweza kujitokeza, NEC na ZEC zitende haki na zihakikishe mawakala wa vyama wana uwakilishi na wanaruhusiwa kuona mchakato mzima wa kura za diwani, mbunge na rais.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kupuuza utabiri TMA madhara ndiyo hayo

Na Faustine Feliciane

MVUA iliyonyesha kwa siku mbili jijini Dar es Salaam, wiki iliyopita imeacha athari kubwa kwa wakazi wa jiji hilo kubwa la kibiashara na cha kusikitisha ni watu kupoteza maisha yao.

Mpaka jana idadi ya watu waliopoteza maisha kutokana na mvua hizo ilifikia 13, Kamanda wa Kanda Maalum ya Kipolisi Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, akithibitisha kutokea vifo hivyo.

Watu wamekufa kutokana na mvua hizo huku waathirika wakubwa wakiwa ni wakazi wa maeneo hatarishi kama vile wakazi wa mabondeni na maeneo ambayo yamekuwa na miundombinu dhaifu na duni hasa madarasa na nyumba.

Mbali na vifo, mvua hizo zimeacha athari kubwa kwenye miundo mbinu pamoja na uharibifu mkubwa wa makazi ya kwa baadhi ya maeneo.

Zipo barabara zilizoharibika, madaraja yaliyokatika na kusombwa na maji, lakini kuna nyumba za wananchi ambazo nazo zimebomoka au kuzingirwa na maji na kusababisha uharibifu wa mali.

Licha ya Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) kutoa utabiri wa mvua katika vipindi tofauti wananchi wamekuwa wagumu kuzifuatilia taarifa zao na kuchukua tahadhari au kufuata maelekezo.

Kwa kiasi kikubwa TMA imekuwa ikitoa taarifa zake karibu kila wakati huku wakiwa na utabiri wa siku, wa saa na utabiri wa jumla.

Maboresho yao katika kutoa taarifa kumefanya mabo wanayoyaeleza kuwafikia wananchi kwa wepesi kwa iwe ni kwa kupitia vyombo vya habari na hata simu za mkononi.

Utabiri unaotolewa na TMA ni kwa ajili ya wananchi kuchukua tahadhari na kujiepusha na uwezekano wa kuwa waathirika wa hali ya hewa na pale kunapoonekana kuna athari kubwa zinazotarajiwa, ni vyema kwa wananchi kuhakikisha wanafuatilia taarifa za TMA, mamlaka mahususi inayotoa habari za hali ya hewa hapa nchini.

Wakati wowote kuanzia sasa TMA inatarajia kutoa utabiri mwingine wa mwenendo wa hali kwa mikoa inayopata mvua mara moja kwa mwaka, ingawa bado haijafahamika utakuwaje, ni vyema wananchi wa mikoa hiyo wakafuatilia kwa ukaribu na umakini taarifa za utabiri zitakazotolewa na mamlaka hiyo na kuchukua hatua.

Athari nyingi zinazotokana na mvua kubwa au ndogo kwa asilimia kubwa zinatokana na wananchi kutofuatilia taarifa za TMA na kushindwa kuchukua tahadhari pale inapobidi.

Ni vyema kukumbushana kuwa wananchi ambao mikoa yao inapata mvua mara moja kwa mwaka ambao utabiri wa mamlaka hiyo utawahusu na ni mahasusi kwa ajili yao kuchukua tahadhari na taarifa zitakazotolewa.

Baadhi ya mikoa ambayo itaguswa na utabiri huo ni Kigoma, Tabora, Rukwa, Katavi, Mbeya, Singida, Songwe, Njombe, Iringa, Lindi, Dodoma,

Mtwara na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro.

Wananchi wa mikoa hiyo pamoja na viongozi wake ni vyema kuzifanyia kazi taarifa za utabiri zitakazotolewa na TMA kesho ili kujiweka katika mazingira bora kutokutana na madhara makubwa yatakayotokana na utabiri wake.

Sera na taratibu za serikali kwa sasa zinaelekeza wahusika wa masuala ya majanga katika mikoa ambao ni makatibu tawala wa mikoa (RAS) pamoja na kamati zao za maafa na usalama hivyo kamati hizo za maafa chini ya makatibu tawala wafuatilie na kuchukua hatua utabiri utakaotolewa na TMA.

Lengo ni hili kuwawezesha wananchi kufahamu kinachoendelea na kuchukua tahadhari.

Inawezekana madhara yaliyotokea mkoa wa Dar es Salaam baada ya mvua kubwa ya siku mbili yametokana pia na tabia ya kutochukua tahadhari pale TMA inapotoa utabiri wake.

Wananchi ni vyema kuacha kupuuza taarifa hizo za TMA ili kuepuke hatari iwe kubwa au ndogo inayoweza kutishia maisha papo kwa papo au baadaye.

Mikoa ambayo utabiri huo utahusika usizifanye masihara taarifa zitakazotolewa na TMA ili kuepuka madhara ambayo yameshuhudiwa Dar es Salaam na maeneo mengine.

## HABARI KITAIFA

# Mgombea urais NRA ataka mdahalo na Lissu

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama cha NRA, Leopold Mahona, ameomba mdahalo kati yake na mgombea urais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, ili aweze kupimana naye ubavu katika kujenga hoja zenye mashiko.

Ametoa ombi hilo jana wakati akizungumza katika mahojiano maalum na gazeti hili kuhusu changamoto alizozibaini katika siku 53 hadi sasa tangu kuanza kwa kampeni za uchaguzi mkuu zilizoanza Agosti 26, mwaka huu.

"Naomba kama kuna 'media' ambayo inaweza kuandaa mdahalo na Tundu Lissu ili nione je, hizo pointi anazosema anaweza kuzitetea vizuri au ni maneno ya jukwaani tu, maana kuna maneno ya jukwaani na maneno ya utendaji," alisema.

Mahona alisema inasikitisha hadi uchaguzi unakaribia kumalizika hakuna hata chombo chochote cha habari ambacho kimejitokeza kutaka kuandaa mdahalo kati yake na Lissu.

Alisema tatizo kuna kasumba kwa media hapa nchini kung' ang'ania kutaka kufanya midahalo na wagombea wa vyama vinavyojipambanua kuwa ni vikubwa kitu ambacho kimsingi siyo cha kidemokrasia kwa sababu vyama vyote viko sawa.

"Kwa muda mrefu nimekuwa nataka nifanye mdahalo na Lissu lakini nimekuwa natafuta fursa siipati," alisema.

Mahona alisema katika kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka huu, vipo baadhi ya vyombo vya habari yakiwamo magazeti na televisheni ambavyo haviandiki wala kutangaza habari za baadhi ya wagombea jambo ambalo linatia ukakasi katika demokrasia nchini.

Aliongeza kuwa kama taifa moja tunatakiwa kuwa kitu kimoja kwa kutengeneza mazingira ambayo yataleta ushindani wa huru na wa haki.

"Tunataka uwanja wa demokrasia katika siasa uwe sawasawa, haiwezekani mgombea mmoja anapewa zaidi kipaumbele kwenye vyombo vya habari wakati Sheria ya Gharama za Uchaguzi ipo wazi," alisema.

Septemba mwaka huu, mgombea urais kupitia CHADEMA, Lissu, alikuwa akisisitiza kwenye mikutano yake ya kampeni akitaka afanye mdahalo na mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Rais John Magufuli.



Wadau wa sekta binafsi wakifuatilia mkutano maalumu ulioandaliwa na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) ili kumpongeza Rais John Magufuli kwa jitihada zake katika kuiboresha sekta hiyo katika kipindi cha miaka mitano. Wa tatu kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (wa tatu kulia) na Meneja Mahusiano Serikalini wa benki hiyo, William Kallaghe (wa pili kulia). **MPIGAPICHA WETU**

# PM mgeni rasmi Baraza la Maulid

**Na Beatrice Moses,TUDARCo**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye Baraza la Maulid kitaifa litakalofanyika katika viwanja vya Karimjee, jijini Dar es Salaam Oktoba 29, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Shekhe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum, alisema Maulid ya mwaka huu inaongozwa na kaulimbiu: 'Uislamu ni amani umoja na mshikamano'.

Shekhe Salum alisema Baraza la Maulidi kitaifa litaanza siku hiyo saa nane mchana hadi zaa 12 jioni na itakuwa siku ya mapumziko, hivyo viongozi wengine mbalimbali wakiwamo wa serikali, mabalozi na wanasiasa wanatarajiwa kuungana na Waislamu wengine kuadhimisha siku hiyo muhimu.

Alisema Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Dar es Salaam na waumini wa dini hiyo jijini hapa wametajwa kuwa ndiyo wenyeji wa Sherehe za kuzaliwa kwa Mtume Mohammad (S.A.W) kitaifa mwaka huu, sawa na mwaka 1442 Hijiria mwaka wa Kiislamu.

Shekhe Salum alisema BAKWATA Dar es Salaam imetoa wito kwa Waislamu kuhudhuria sherehe za awali za Maulid ambazo zinawakumbusha maisha matukufu na historia ya kiongozi wao muasisi wa umma wa Kiislam aliyewaletea heshima na utukufu na kumkomboa binadamu.

Alisema kuwa kwa mujibu wa Mufti wa Tanzania, Shekhe Abubakar Bin Zuber Bin Ally, sherehe hizo kitaifa zinatafanyika kesho (Jumatano) saa 2:30 usiku hadi saa 5:30 usiku katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini hapa.

"Sawa na usiku wa mwezi 12 mfungo sita 1442 Hijiria, ambayo Waislamu toka mikoa mbalimbali nchini na nje ya nchi watajumuika pamoja na wenzao wa Mkoa wa Dar es Salaam kuonyesha heshima na mapenzi yao kwa Mtume Mohammad (S.A.W)," alisema.

# Samia ahimiza ushirikiano taasisi za fedha, sekta binafsi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais Samia Suluhu, ametoa wito kwa kwa taasisi za kifedha kushirikiana na wadau wa sekta binafsi ili kukuza mitaji yao na kuongeza ushindani wa kibiashara dhidi ya wenzao kutoka nje.

Samia alitoa wito huo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na wadau mbalimbali wa sekta binafsi waliohudhuria Mkutano maalumu ulioandaliwa na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) jijini Dar es Salaam ili kumpongeza Rais John Magufuli kwa jitihada zake katika kuiboresha sekta hiyo katika kipindi cha miaka mitano.

"Pamoja na ubora wa sera zinazoongoza sekta binafsi bado serikali tunaamini kwamba weledi kwenye utoaji wa huduma za kifedha nchini bado ni nguzo muhimu katika kufanikisha ustawi wa sekta ya binafsi. Niyaombe sana mabenki yetu tusaidiane kwenye hili," alisema Samia.

Akizungumza kwenye hafla hiyo Mweyekiti wa Bodi ya TPSF, Angelina Ngalula pamoja na kumpongeza Rais Magufuli kwa uimara aliouonesha katika kipindi cha miaka mitano katika kuisaidia sekta hiyo, alizipongeza taasisi za fedha nchini kwa namna zinashirikiana na sekta binafsi katika kukuza mitaji ya wadau hao.

"Baadhi ya taasisi hizi zimekuwa hazishii katika kutoa mikopo tu bali pia zimekuwa zikitusaidia katika kufanikisha mikakati yetu ikiwamo mikutano muhimu inayolenga kujadili fursa na mipango muhimu kwa ustawi wetu", alisema huku akizipongeza taasisi hizo miongoni mwao ikiwamo benki ya NBC ambayo ni moja ya wadhamini wakuu wa mkutano huo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa benki ya NBC, Theobald Sabi, alisema benki hiyo imejipanga zaidi kushirikiana na sekta binafsi pamoja na serikali ili kusukuma maendelea ya sekta hiyo, huku akiweka wazi baadhi ya mikakati na huduma ambazo benki hiyo inazitoa kwa wadau wa sekta binafsi.

Alisema ustawi wa sekta binafsi nchini unategemea huduma bora za kifedha zinazoendana na mahitaji halisi ya wadau hao.

"Ndio maana benki ya NBC tumekuwa karibu sana na wadau wa sekta binafsi si tu katika kutoa huduma bali pia kushirikiana nao katika kufanikisha mikakati yao mbalimbali kwa kuwa tunaamini kupitia ushirikiano na ukaribu huu tunaweza kufahamu zaidi mahitaji yao hatua inayotuwezesha pia kubuni huduma zinazoenda sambamba na mahitaji yao," alisema Sabi ambae benki yake hiyo ilikuwa ni moja wa wadhamini wakuu wa mkutano huo.

Aidha alitaja baadhi ya huduma na mikakati ya benki hiyo katika kuwasaidia wadau wa sekta binafsi kuwa ni pamoja na uendeshaji wa kliniki za biashara kwa wafanyabiashara wakubwa na wa kati kupitia ushirikiano baina ya benki hiyo na TANTRADE pamoja na utoaji wa mikopo na mafunzo kwa wajasiriamali.

# Polisi waua wawili madai ya ujambazi

**Na Allan Isack, ARUSHA**

> **"Kwa kuwa siku hiyo, kulikuwa na giza upekuzi ulifanyika tena asubuhi ya Oktoba 18, kwa kushirikiana na wananchi tulifanikiwa kuzipata silaha mbili aina ya Bastola aina ya Bereta isiyokuwa na namba ikiwa na risasi nne ndani ya magazine," alisema Hamduni.**

JESHI la Polisi Mkoa wa Arusha, limewaua watu wawili wanaotuhumiwa kuwa ni majambazi.

Watuhumiwa wengine watatu wa ujambazi, wanadaiwa kukimbia wakati wa jeshi hilo likiendelea na shughuli ya upekuzi katika eneo la tukio, ilikopatikana silaha moja aina ya Shotgun ikiwa na risasi tisa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi, Salum Hamduni, alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 18, mwaka huu, majira ya saa 1:30 mchana katika eneo la Olkerian Kata ya Moshono jijini Arusha.

Kamanda Hamduni, aliwataja watuhumiwa hao, wa ujambazi kuwa ni Bashiri Ally na mtuhumiwa mwingine alifahamika kwa jina moja la Mohamed.

Alisema kuwa baada ya watuhumiwa hao, kutaka kukimbia polisi walifyatua risasi juu kuwaonya wasikimbie badala yake waliendelee kukimbia na walianza kurushiana risasi na askari polisi, hali iliyosababisha Bashiri Ally, kujeruhiwa sehemu za miguu na mgongoni.

Alisema baada ya kurushiana risasi na askari polisi walijeruhiwa na wakati wakipelekwa hospitalini kwa ajili ya kupatiwa matibabu walifariki dunia.

Hata hivyo, alisema kabla ya umauti Mohamed akiwa anapelekwa hosipitali alihojiwa na kuwataja watuhumiwa wengine watatu majambazi waliotoroka, pia walieleza kuwa walikuwa na silaha nyingine mbili aina ya bunduki (shotgun) na bastola waliziangusha katika eneo la tukio wakati wakirushiana risasi na askari polisi.

"Kwa kuwa siku hiyo, kulikuwa na giza upekuzi ulifanyika tena asubuhi ya Oktoba 18, kwa kushirikiana na wananchi tulifanikiwa kuzipata silaha mbili aina ya Bastola aina ya Bereta isiyokuwa na namba ikiwa na risasi nne ndani ya magazine,"alisema Hamduni.

Aidha, alisema jeshi hilo, linaendelea na msako ili kuwakamata watuhumiwa waliotoroka katika tukio hilo, pia jeshi la polisi limewaomba wananchi kutoa taarifa ili kufanikisha shughuli ya kuwakamata wahusika hao.

# Wafungwa miaka 30 jela kwa unyang'anyi wa kutumia silaha

**Na Samson Chacha, TARIME**

> **Alidai watuhumiwa hao walimvamia na kumweka chini ya ulinzi huku wakimtishia silaha jadi mapanga, Yokabe Mohere na kumnyang'anya Simu aina ya Tecno yenye thamani ya Sh. 300,000, Hassan Wanchara**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Tarime mkoani Mara, imewahukumu miaka 30 jela wakazi wawili wa Mtaa wa Rebu Tarime Mjini, Masana Mairo (33) Tito Yohana Misaku (30), baada ya kupatikana na hatia ya wizi wa kutumia silaha.

Watuhumiwa hao walikutwa na hatia ya kufanya wizi wa kutumia silaha katika matukio matatu tofauti kwa kupora watu watatu zaidi ya Sh. 600,000 na simu nne za mkononi.

Awali, mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Wilaya Tarime, Charles Mnzava, Mwendesha mashtaka wa Serikali, Peter Ilole, alidai kuwa watuhumiwa hao walitenda kosa hilo usiku wa Oktoba 21, mwaka huu katika Mtaa wa Mtaa wa Rebu kwa kutumia wakiwa na silaha za jadi kama mapanga, marungu na nondo.

Alidai kuwa watuhumiwa hao waliwavamia, kuwatishia na kuwajeruhi wananchi watatu katika matukio matatu tofauti usiku huo na

kuwanyang'anya fedha zaidi ya Sh. 600,000 na simu za mkononi nne.

Alidai watuhumiwa hao walimvamia na kumweka chini ya ulinzi huku wakimtishia silaha jadi mapanga, Yokabe Mohere na kumnyang'anya Simu aina ya Tecno yenye thamani ya Sh. 300,000, Hassan Wanchara aliyenyang'anywa Sh. 130,000 na simu aina ya Aitel yenye thamani ya Sh. 30,000.

Mwingine aliyeporwa fedha kiasi cha Sh. 105,000 na Simu aina yaTecno yenye thamani ya Sh. 50,000 ni Jumapili Mosae, na kwamba aliwatishia kwa silaha walizokuwa nazo.

Aidha, aliiomba Mahakama hiyo kuwapa adhabu kali ili iwe fundisho na kukomesha vitendo hivyo vinavyoanza kushamiri na kuumiza watu.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mnzava alisema baada ya kujiridhisha na ushahidi wa pande zote mahakama imeamua kuwahukumu miaka 30 jela kila mmoja.




HABARI KITAIFA

# Ushirikiano wa serikali, kampuni ugawaji wa mbolea

**Na Mwandishi Wetu**

Kampuni ya YARA Tanzania imeahidi kushirikiana na serikali kwa karibu ili kuhakikisha mpango wa ugawaji mbolea bure kwa wakulima nchini unakuwa wa manufaa kwa wakulima na taifa kwa jumla.

Akizungumza na waandishi wa habari siku chache baada ya uzinduzi wa ugawaji wa mbolea uliofanyika jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Winstone Odhiambo, alisema mpango huo umelenga kuhakikisha nchi za Afrika ikiwamo Tanzania zinajitosheleza katika kuzalisha chakula.

Kwa upande wa Tanzania mpango huo ni jitihada ya kampuni yao kuchangia jitihada ya serikali katika kuimarisha sekta ya kilimo.

"Lengo la kampuni ni kuhakikisha uzalishaji wa mazao hususani mahindi na mpunga unaongezeka katika nchi za Afrika kupitia mradi maalum wa kampuni ujulikanao kama Action Africa,"alisema Odhiambo.

Alisema mradi wa ugawaji mbolea bure ni moja ya miradi mikubwa ambayo imetekelezwa tangu kampuni kuanzishwa nchini Tanzania miaka 15 iliyopita.

"Naishukuru Serikali ya Tanzania, kupitia Wizara ya Kilimo, kwa ushirikiano mkubwa tulioupata ambao umetusaidia kuhakikisha azma ya kampuni yetu inatekelezeka kwa vitendo na pia kwa kufanya tafiti za ubora wa mbolea kupitia mamlaka za uthibiti zilizopo nchini," alisema Odhiambo.

Aliongezea ubora wa mbolea inayotolewa kwa wakulima umezingatia mazingira ya ardhi ya Tanzania na kuongeza kwamba mbolea hiyo itatibu udongo na kurutubisha aradhi na kwa hiyo mazao yatastawi vizuri na kuongezeka.

"Mbolea inayokwenda kwa wakulima ni NPK ambayo ni mahsusi kwa mazao ya mpunga na mahindi, hivyo tani 12,500 zitagagiwa kulingana na vigezo na masharti yaliyowekwa," aliongeza.

Alieleza kuwa mpango huo mbali ya kuongeza chakula, ni sehemu pia ya kuunga mkono juhudi za Serikali ya Rais John Magufuli katika kuendeleza kilimo ili kiweze kusaidia katika maono ya nchi ya kufikia uchumi wa viwanda ifikapo 2025.

**Mbolea inayokwenda kwa wakulima ni NPK ambayo ni mahsusi kwa mazao ya mpunga na mahindi, hivyo tani 12,500 zitagagiwa kulingana na vigezo na masharti yaliyowekwa.**

# Mgombea CHADEMA ajinadi kukomesha udumavu watoto

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MGOMBEA ubunge Jimbo la Kibaha Mjini kwa tiketi ya Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Michael Mtally, amesema akipata ridhaa ya kuongoza jimbo hilo kati ya mambo atakayoyapa kipaumbele kuyashughulikia ni pamoja na udumavu kwa watoto.

Mtally alisema njia ya kwanza atakayoitumia ni pamoja na kutoa elimu kwa wazazi na walezi kuhusu lishe bora kwa watoto wao na familia kwa ujumla ili wakawe imara kiafya na asiwapo anayekabiliwa na udumavu.

Mgombea huyo alisema, atasimamia pia utoaji wa elimu ya ujasiriamali kwa kundi la wazazi na walezi ili wakidhi sifa za kujiunga kwenye vikundi na kukopesheka wajishughulishe na biashara zitakazowawezesha kumudu kupata lishe bora.

**Ili kutokomeza hali ya udumavu katika Halmashauri hiyo wamejipanga kutoa elimu ya lishe kwa vitendo kwa jamii.**

" Kuna baadhi ya maeneo katika jimbo letu bibi ndio analea wajukuu, lakini pia ukiangalia hali zao kimaisha ni duni wanatakiwa kuwezeshwa kiuchumi waunganishwe kwenye vikundi wanufaike na mikopo ya kufanya biashara ndogo dogo zitakazowakwamua kiuchumi na kupata lishe bora nyumbani kwao," alisema.

Alisema amelazimika kuweka mkakati huo baada ya kubaini baadhi ya familia walezi wa watoto ni mabibi wanaoachiwa kulea wajukuu, huku wakiwa na uwezo duni kiuchumi.

Akizungumzia kuhusiana na hali ya udumavu katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Ofisa Habari, Innocent Byarugaba, alisema ni asilimia 0.02 pekee kwa watoto wenye udumavu, ambapo hivi karibuni takwimu za Mkoa zilieleza kuwa ni asilimia 23.

Byarugaba alisema ili kutokomeza hali ya udumavu katika Halmashauri hiyo wamejipanga kutoa elimu ya lishe kwa vitendo kwa jamii.

Aidha, alisema mkakati mwingine katika Halmashauri hiyo ni kuanzisha siku ya afya na lishe katika mitaa na upimaji wa hali ya lishe kwa watoto chini ya miaka mitano kwa kutumia wahudumu wa afya ngazi ya jamii.



Kazi wa jijini Dar es Salaam akipita kwa shida kutokana na matope yaliyosababishwa na mvua zilizonyesha katika eneo la stedi Kawe. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mil. 72/- kuwanunulia mbolea bure wakulima vijana Kahama

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, imetenga kiasi cha sh. milioni 72 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya kununua pembejeo na kuzigawa bure kwa wakulima vijana wenye uwezo wa kulima kuanzia hekari tano.

Lengo la utoaji wa pembejeo hizo kwa wakulima vijana katika kata 20 za halmashauri hiyo ni kuongeza uzalishaji katika mazao ya kimkakati hasa mpunga, elizeti, mahindi na pamba.

Lengo lingine la mpango huo ni kupunguza wimbi la vijana mitano wasiokuwa na shughuli za kufanya.

Mwaka juzi halmashauri ilitenga kiasi cha Sh. milioni 54 na kutumika kiasi cha Sh. milioni 14.19, kutokana na mwitikio wa wakulima vijana ulikuwa chini, na wakulima walionufaika na pembejeo bure walikuwa 27 na kulima zaidi ya hekari 139.

Pia mwaka jana Halmashauri ilitenga kiasi cha Sh. milioni 17.9 na kununua mbolea za kupandia (NPK) kilo 195, mahindi kilo 550, mbegu za alizeti kilo 90 na sumu ya kuua wadudu wanaoshambulia pamba chupa 90 na kuzigawa kwa wakulima 39 waliolima hekari 195.

Hayo yalibainishwa jana na Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Samsoni Sumuni, wakati akizungumza na gazeti hili, ambapo alisema kuwa vijana wanaonufaika na mkopo wa pembejeo bure ni wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 35 na kulima hekari tano za mazao na kuendelea.

"Kila mwaka wa fedha tumekuwa tukitenga fedha za kununua pembejeo na kuzigawa bure kwa wakulima vijana, na kila mwaka tumekuwa tukiwapatia vijana tofauti. Tunaongeza uzalishaji katika mazao ya kimkakati na mazao wanayoyapata ni mali yao nasio mali ya halmashauri," alisema Sumuni.

Aidha, Sumuni alisema wanatarajia kununua pembejeo za NPK mbegu za mahindi, sumu ya kuua wadudu wanaoshambulia pamba, miche ya mitunda pamoja na mbegu zinazostamili ukame.

Kwa sasa uzalishaji uongezeka kutoka gunia saba za mahindi hadi gunia 25 kwa hekari moja na kutoka gunia nane hadi gunia 25-30 kwa hekari moja ya mpunga, hali ambayo imetokana na msimu uliopita mvua kuwa za kutosha.

Salumu John, mkazi wa Kata ya Kinaga, alisema vijana wengi wanashindwa kujikita kwenye kilimo kwa sababu ya ukosefu wa fedha za kununua pembejeo.

# Maofisa elimu waagizwa bajeti taulo za kike

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERIKALI mkoani Shinyanga imewaagiza maofisa elimu wa halmashauri zote sita za mkoani humo wa shule za msingi na sekondari, kuhakikisha wanatenga bajeti kila mwaka wa fedha, kwa ajili ya kununua taulo za kike (pedi), ili kuwasaidia wanafunzi wa kike wasio na uwezo kutokosa masomo wanapoingia kwenye siku zao.

Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Shinyanga, Joachim Otaru, alitoa agizo hilo juzi wakati akifunga mafunzo ya afya ya uzazi na malezi, na kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa viongozi wa klabu za wanafunzi kutoka shule 18 za msingi na sekondari mkoani humo.

**Washtakiwa wataendelea kuwa rumande kutokana na makosa yanayowakabili kutokuwa na dhamana.**

Alisema anasikitishwa kuona suala la taulo za kike limebaki kutekelezwa na wadau pekee, wakati jukumu hilo ni la Serikali, na kuwataka maofisa elimu wa halmashauri kuweka utaratibu wa kutenga bajeti kila mwaka wa fedha, kwa ajili ya kununua taulo la kike na kuzisambaza mashuleni.

"Shirika la World Vision limetusaidia maboksi 424 ya taulo za kike, kwa ajili ya kuwastiri wanafunzi wanapokuwa katika siku zao, ambapo takwimu zinaonyesha kila mwaka mwanafunzi wa kike lazima akose masomo ndani ya miezi miwili anapokuwa kwenye hedhi kwa kukosa taulo hizi," alisema Otaru.

Naye Mratibu wa mradi wa kuboresha afya wa (ENRICHO) unaotekelezwa na Shirika la World Vision, Dk. Frank Mtimbwa, alisema mbali na kutoa taulo za kike kwa wanafunzi, pia wametoa msaada wa runinga nane, vifaa vya michezo jezi pea 72, na mipira 72, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 62.8.

Mmoja wa wanafunzi walioshiriki mafunzo hayo, Nchambi Elias kutoka Shule ya Sekondari Mangu wilayani Kishapu, alishukuru msaada huo wa taulo za kike, na kubainisha hiyo imekuwa ni changamoto kubwa kwa wanafunzi ambao hawana uwezo wa kuzinunua, hivyo kukosa masomo kila wanapoingia kwenye siku zao.



Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, Asia Abdallah, akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Ilawa katika Kata ya Image wilayani Kilolo, mkoani Iringa kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo wakati ya ziara yake ya kusikiliza kero zao juzi. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

## Jacob ajinadi kuendeleza miradi Ubungo

**Na Enock Charles**

MGOMBEA ubunge katika jimbo la Ubungo jijini Dar es Salaam kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA),Bonifasi Jacob, ameahidi kuendeleza miradi aliyoianza wakati akiwa Meya wa Ubungo.

Miongoni mwa miradi hiyo ni uboreshaji wa barabara, kuongeza shule za msingi katika baadhi ya kata zenye upungufu na uboreshaji wa zahanati.

Akizungumza na wananchi wa Kata ya Msewe mwishoni wa wiki iliyopita kwenye mkutano wa kampeni, mgombea huyo alijigamba kwamba akiwa Meya katika Manispaa ya Ubungo ambayo ipo katika jimbo hilo, yapo mambo mengi aliyoyafanya katika na kueleza kuwa iwapo atapewa ridhaa ya kuliongoza jimbo hilo atayaendeleza.

"Nilipokuwa Meya, barabara ya NIT kwenda Mburahati ilikuwa mbovu, nimeshiriki kuitengeneza kwa kuisimamia TARURA,nikienda Msewe nitasema nimejenga zahanati,nikienda Sinza nitawaambia tumeboresha Zahanati ya Sinza kuwa Hospitali ya dharura ya Wilaya," alitamba Jacob.

Meya huyo wa zamani wa Ubungo alidai kuwa licha ya kwamba hakumalizia ngwe yake ya uongozi baada ya kufanyiwa kile alichokiita hujuma, lakini alijitahidi kutekeleza ahadi zake zote na kuwaahidi wananchi wa Ubungo kufanya kazi zaidi iwapo atachaguliwa kuwa mbunge katika jimbo hilo.

Kampeni za kuwania nafasi za udiwani, ubunge na urais zinaelekea ukingoni ambapo sasa zimesalia siku nane tu kabla ya wananchi kufanya uamuzi Oktoba 28, mwaka huu.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC)ilitangaza kuwapo na vituo vya kupigia kura 80,155 huku waliojiandikisha ni 29,188,347 ambao watachagua wabunge 390 na madiwani 5,350.

Kampeni za Uchaguzi zilipangwa kufanyika kwa siku 64,huku kila mgombea akitoa ahadi ya kuleta mabadiliko au kuendeleza yaliyofanyika.

# Sekta binafsi yatoa neno ujenzi wa miundominu

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU wa Sekta Binafsi wamepongeza ujenzi wa miundombinu ikiwemo reli ya kisasa (SGR) na bwawa la ufuaji umeme vitasaidia kuchochea fursa za uwekezaji hususani kwenye viwanda kwenye maeneo mbalimbali.

Akizungumza katika mkutano ulioandaliwa na Taasisi na Taasisi ya Sekta Binafsi hapa nchini (TPSF),kwa lengo la kuipongeza serikali kwa mchango wake mkubwa wa kuinua sekta binafs jijini Dar es Salaam juzi, Mwenyekiti wa Taasisi ya sekta hiyo, Angelina Ngalalu, alisema ujenzi wa miundombinu ni miongoni mwa mafanikio makubwa katika kuinua uchumi wa taifa.

"Kwa miaka mitano Serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Magufuli imefanya makubwa sana na yenye tija kwa uchumi wa Taifa, tunaamini kama wawekezaji tutatumia kila fursa inayopatikana kufanya uwekezaji kulingana na mazingira mazuri yaliyowekwa na serikali," alisema Ngalula.

Alisema kuwa ujenzi wa reli ya kisasa na miundombinu mingine kama bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere litakalozalisha megawati 2,115 utaongeza soko la ajira kwa vijana wa Kitanzania na hivyo kuchangia ukuaji wa pato la taifa.

"Katika kipindi cha miaka mitano tumeshuhudia ujenzi wa miundombinu ya kimkakati ambayo imechangia upatikanaji wa ajira kwa vijana wa Kitanzania na ajira zaidi zitakuja punde ujenzi wa miundombinu hiyo utakapokamilika kwa kuwa wadau wa sekta binafsi watawekeza katika miundombinu hiyo," alisema.

Alisema ujenzi wa reli hiyo utaongeza kiwango cha mizigo itakayosafirishwa kutoka tani milioni tano kwa mwaka kwa sasa na kufikia tani milioni 14 kwa mwaka.

"Ujenzi wa SGR utasaidia kuongeza kiwango cha mizigo itakayosafirishwa kutoka tani milioni tano kwa mwaka kwa sasa hadi tani milioni 14 kwa mwaka pindi ujenzi utakapokamilika," alisema na kuongeza kuwa hali hiyo itaongeza tija kwenye uchumi na ukuaji wa biashara kwa nchi.

Aidha ameiomba serikali kuendelea kutoa ushirikiano kwa Taasisi hiyo kama ambavyo imefanya kwa kipindi chote cha miaka mitano ili kujenga uchumi imara na wenye kuleta tija kwa wananchi.

"Katika nchi nyingi zilizoendelea zilifanya hivyo kwa kuweka mazingira rafiki ili wadau wa sekta binafsi waweze kufanya uwekezaji."

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Waendesha bodaboda nchini, Michael Haule, alisema kupitia vikundi vyao wamepata bima ya afya kwa gharama nafuu.

Nipashe

# TESA

Jumanne Oktoba 20, 2020

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 12

**Uhamiaji inavyowarejesha mabinti darasani**



Ukurasa 13

300 waliokuwa wasisome wapata neema



Ukurasa 14

**Ni faida lukuki kilimo ikolojia**

TEKNOLOJIA

NA NIMI MWETA

# Wataalamu wanaposhtuka nishati mbadala kiama mazingira, dunia



Mapangaboi ya umeme wa upepo ni miongoni mwa miundombinu ya kuzalisha nishati inayotajwa kuwa si salama kwa mazingira ya dunia. **PICHA: MTANDAO**

KWA miongo kadhaa dunia imeaminishwa kuwa tiba ya uchafuzi wa mazingira na uharibifu wa tabaka la ozone ni kuacha kutumia nishati za visukuku kama makaa ya mawe na mafuta ya kuchimba ardhini, badala yake kuegemea nishati jadidifu (renewable energy).

Hata hivyo, imani kwenye nishati jadidifu za maji, jua na upepo hiyo inaanza kutiliwa shaka kutokana na ukweli kuwa uzalishaji wake ni kiama kwani unategemea malighafi za hatari kuliko visukuku.

Nishati za visukuku ni zile zinazotokana na mabaki ya wanyama na mimea (fossils) yaliyofunikwa ardhini kwa maelfu ya miaka ambazo ni makaa ya mawe, mafuta na gesi za kuchimbwa ardhini.

**CHANZO CHA WASIWASI**

Hofu ya nishati jadidifu kama maji, upepo na maji zimeanza kuleta shaka, baada ya kubaini kuwa vifaa vinavyohitajika ili kuunda 'mapangaboi makubwa' ya kuzalisha umeme wake vinategemea sana aina kadhaa za vyuma adimu, unaoelezwa kuwa upatikanaji wake una madhara ya kutisha.

Kwa miaka kadhaa wataalamu wamekuwa wakiibua maswali kuhusu uendelevu wa nishati mbadala, baada ya madhara kuanza kutajwa katika maeneo yanayopatikana madini ya kutengeneza vifaa hivyo.

**TISHIO LA MAZINGIRA**

Kwa mujibu wa makala ya utafiti kuhusu uchimbaji wa bati na madini adimu nchini China na shaba inayopatikana Chile inayorushwa na Televisheni ya Al Jazeera, kuna uharibifu wa kutisha wa mazingira unaoonekana katika nchi hizo, unaosababishwa na kusaka madini hayo.

Na haikuwa utafiti wa siri ila wataalamu katika taasisi husika na mamlaka nyingine za usimamizi mazingira walikuwa wanakiri hivyo.

**MAFUTA, GESI KUENDELEA**

Katika nchi za Magharibi kusambaza na kutafiti zaidi hoja dhidi ya kile kinachoitwa nishati jadidifu kunaonyesha kuwa matazamio ya dunia kujikomboa na mafuta kutokana na uzalishaji wa hewa ukaa (carbon dioxide) kama utatuzi wa suala zima la mazingira ni bomu la kutegwa.

Kwa kuhamia katika nishati mbadala, dunia sasa inaingia katika utegemezi mpya wa vyuma adimu ambavyo upatikanaji wake kwa viwango vya kutosha na kwa bei inayofaa ni kitisho kwa kimazingira.

Tatizo la nishati endelevu katika utafiti huu ni jinsi ambavyo takriban kila kinachohitajiwa katika kuzalisha umeme wa upepo wa jua na mimea (bioanuwai) siyo kisafi kina athari zaidi.

Makala ya televisheni Al Jazeera iliyonyesha maeneo makubwa ya jangwa ambako uchimbaji wa bati na shaba unaotumia maji mengi ya kawaida umeharibu vyanzo vya maji sehemu kubwa tu za China na Chile.

Katika eneo la 'jangwa la shaba' huko Chile, ripoti ilisema haijanyesha mvua kwa miaka 500 sasa.

Ina maana kuwa ukiangalia kwa karibu, ni rahisi zaidi kwa dunia kutafuta njia za kukabiliana na athari za matumizi ya makaa ya mawe na mafuta ya kuchimbwa, kuliko kutegemea upatikanaji kwa wingi wa vyuma adimu.

Aidha, umeme wa nishati mbadala unaonekana kuwa hauna tija ya kutosha kuwa mbadali wa mafuta na hata wa nuklia, kwa sababu unahitaji vifaa vingi kwa uzalishaji lakini kinachopatikana ni umeme mdogo inapolinganishwa na ule wa mafuta, makaa au gesi.

Kwanza, vifaa vya kutafutia madini ya vyuma adimu ambavyo vinatumika kusuka 'jenereta' na mabangaboi makubwa ya umeme mbadala hasa mashine za uchimbaji wa madini hayo na usafirishaji wake vinategemea matumizi ya mafuta ya kawaida na mafuta mazito.

Ina maana kuwa hapatakuwa na afueni ya wazi au ya haraka kwani matumizi ya mafuta yanayozalisha gesi chafu yatabadilika kiasi tu, lakini hayakwepeki katika kazi nzito za kuzalisha nishati au kutafuta madini.

Kinachoongezeka ni hitaji kubwa mno la madini adimu ya aina tofauti za chuma na bati ambayo yanaharibu mazingira kwa kasi zaidi kuliko mafuta.

Watafiti nchini Marekani wanafafanua suala hilo wakisema kuwa betri moja ya gari la kawaida linalotumia umeme badala ya petrol au dizeli ina uzito wa karibu nusu tani.

Ili kutengeneza betri hiyo inabidi kuchimba na kuchakata mali ghafi ardhini yenye uzito mara 500 ya hiyo betri kutoka popote pale.

Isitoshe, mazingira ya uchimbaji wa madini hayo, ikiwamo afya za wafanyakazi katika mazingira ambayo kuchimba kunalenga kuuza madini hayo kwa bei ya chini kwa mfano inavyofanya China ili kutawala soko.

Kinachoonekana kuwa kikwazo kikubwa zaidi cha nishati mbadala na hasa kwa kutengenezwa vitu 'vinavyong'ara' ni wingi wake na uunganishaji wake kila mahali, kwa mfano gari la umeme kuhitaji nyaya za umeme njia yote inayopitia, si kama kujaza mafuta mara moja.

Isitoshe, wakati vyuma vya kawaida vya magari vinayeyushwa na kutumika kutengeneza vifaa vya chuma au magari mengine, si rahisi kukomboa na kuanza kutumia tena vingi kati ya malighafi au vifaa vinavyotumika katika vyombo vya kielektroniki.

Ina maana kuwa vifaa hivyo haviwezekani kufanyiwa urejelezaji (recycling) kwa urahisi ili kuzalisha bidhaa nyingine.

Mojawapo ya maeneo ya umeme mbadala yaliyofanyiwa utafiti hivi karibuni nchini Marekani katika jimbo la California, ambako wataalamu wanasema jitihada za kutengeneza umeme mbadala kwa wingi zinatishia kufilisi kampuni kubwa ya umeme eneo hilo.

Wanasema sera za nishati mbadala zimeharibu usimamizi na tija katika utengenezaji na usambazaji wa umeme jimboni humo.

Utafiti huo unasema malighafi hizo zinatoka nchi ambazo hakuna anayepaza sauti kuhusu uharibifu wa mazingira na hiyo ni hatari kubwa zaidi.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Uhamiaji inavyowarejesha mabinti darasani

## Inadhibiti pasipoti, waepushwa ukahaba 'majuu'

WASICHANA wanapokuwa shuleni, hukutana na vishawishi vingi kimojawapo ni hadaa za ngono utotoni, lakini pia kupewa ahadi za kupata kazi ughaibuni, kulipwa mishahara kwa Dola na kupata maisha bora huko ng'ambo.

Wengi wanavutiwa kuacha shule na kukimbilia 'majuu' wakiaminika kuwa ajira za ng'ambo zitamaliza changamoto za kimaisha bila kujua kuwa wanakwenda kuwa watumishi wa ndani na wahanga wa biashara za ukahaba, anaeleza Mrakibu wa Uhamiaji Wilaya ya Kisarawe, Rosemary Mkandala,

Mkoa wa Pwani ni miongoni mwa maeneo ambayo wasichana walikuwa wakiacha shule na kutafuta kazi nchi za nje, lakini wengi waliishia kulalamika kwa dhuluma na kutumikishwa kwenye biashara ya ukahaba.

Na ili kuudhibiti, Idara ya Uhamiaji Mkoa, inachukua hatua ikiwamo udhibiti mkubwa wa pasi za kusafiria kwa mabinti, kushirikisha wazazi na walezi kukomesha mazoea ya kuwasafirisha wasichana na kuchunguza sababu zinazotolewa na wazazi na walezi waomba pasi hizo.




Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo (kushoto), katika maadhimisho ya Siku ya Binti Duniani, yaliyofanyika wilayani humo Jumapili Oktoba 11, 2020. **PICHA: MWANDISHI WETU.**

Mrakibu wa Uhamiaji Kisarawe, Rosemary Mkandala, anasema udhibiti unaanzia kwa kuhoji sababu za binti kwenda nje, Aidha, inalinganisha umri , kazi anazodaiwa kwenda kufanya na katika nchi gani.

Anasema hayo kwenye mahojiano na Nipashe wakati wa maadhimisho ya siku ya mtoto wa kike duniani, yaliyofanyika wilayani Kisarawe na kudhaminiwa na vyombo vya habari vya IPP Media pamoja na wadau wengine.

Oktoba 11, maofisa wa Idara ya Uhamiaji Kisarawe, walikita kambi kwenye viwanja vya Sekondari ya Minaki, yalikofanyika maadhimisho hayo, ikiwa ni jitihada za kuelimisha washiriki kuhusu majukumu ya idara hiyo lakini pia, kuhamasisha umma na wasichana kuhusu athari za kutorokea ughaibuni kusaka ajira.

Akiwa chini ya miaka 14 haruhusiwi kuondoka nchini bila mzazi au mlezi kutoa maelezo ya kuthibitika, ikishindikana wengi wanarudishwa kuendelea na masomo, anaeleza Rosemary.

Anaongeza: "Haitoshi kumuombea binti pasi kwa maelezo kuwa anakwenda ng'ambo kwa jamaa zake. Uhamiaji inachunguza kikamilifu kwa kutumia balozi ziliko nje na kutumia pasipoti za sasa zenye taarifa za 'kibayometriki' kujua ukweli wa maelezo ya mwenyeji anayetajwa."

Aidha, ofisi balozi zilizoko nje zinatumiwa kuthibitisha uwapo wa jamaa hao wanaotajwa na kuwachunguza kujua ukweli wa taarifa zinazotajwa kwenye matembezi ya wasichana hao.

Anafafanua kuwa hapo awali wasichana waliweza kupata pasi na kuondoka, huku baadhi ya wazazi na walezi wakitoa maelezo kuwa wanakwenda kutembelea ndugu kama shangazi, mjomba au mwanafamilia yeyote aliyeko nje.

"Zama hizi hilo haliwezekani" anasema na kuongeza kuwa baadhi waliacha shule na kwenda kusaka ajira jambo ambalo, liligundulika baadaye baada ya kuibuka malalamkiko na kuanza uchunguzi na ufuatiliaji.

Ofisa huyo wa Uhamiaji Wilaya ya Kisarawe, anasema ili kumlinda msichana huyo, wazazi, walezi na mwenyeji aliyeko ng'ambo wanabeba dhamana ya usalama, ulinzi na mustakabali mwema wa binti.

Anaongeza kuwa miaka ya nyuma wasichana mkoani humo, waliacha shule na kwenda nchi za nje walikotumikishwa kwenye ukahaba na kazi nyingine zisizothamini utu wa mtu.

"Uhamiaji imewahamasisha wasichana kujua kuwa elimu ni fursa kubwa kwa maisha na kwamba , ukahaba, wala kutumikishwa kazi za ndani siyo kitu cha kikimbilia tena kwa kuacha masomo," anaeleza.

Anafafanua kuwa miaka ya hivi karibuni hamasa zimefanyika katika shule nyingi mkoani zikiwamo Minaki, Pugu, Mwanarumango, Kimani na Chanzige kuwahimiza wasichana na watoto kwa ujumla kusoma na kuachana na fikra kuwa ajira za ng'ambo ni bora kuliko elimu wanayopewa madarasani.

### KUINUA ELIMU

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo Mkurugenzi wa Maendeleo ya Wilaya, Musa Gama anasema Kisarawe inaweka mkazo kwenye elimu ya mabinti na kwamba Mkuu wa Wilaya Jokate Mwegelo, amejenga sekondari ya wasichana.

"Amejenga shule ya sekondari ya wasichana inayojulikana kama Jokate Mwegelo High School iliyoko Muhaga , inayotarajiwa kuanza kusajili wasichana kuanzia Januari mwakani" anasema.

Gama anasema itakuwa ni shule ya bweni itakayokuwa na wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi sita kwa ajili ya wasichana peke yao.

Anaongeza kuwa hizo ni jitihada zinazofanywa na DC kupitia kampeni za 'kutokomeza ziro Kisarawe' na kuvunja ukimya zikiwa ni juhudi za kusaidia wasichana ili wasonge mbele kitaaluma na kuwaepusha na unyanyasaji kijinsia.

> Amejenga shule ya sekondari ya wasichana inayojulikana kama Jokate Mwegelo High School iliyoko Muhaga , inayotarajiwa kuanza kusajili wasichana kuanzia Januari mwakani" anasema.

### CHANGAMOTO KIELIMU

Mkurugenzi wa Maendeleo, Gama akizungumzia changamoto zinazoikabili elimu ya mabinti anataja mimba za utotoni kuwa zipo, akisema mwaka huu kuanzia Januari hadi Oktoba wasichana 43 wa shule za msingi na sekondari wamekuwa wajawazito.

"Katika kukabiliana na unyanyasaji huo washtakiwa walifikishwa mahakamani. Wawili wamefungwa jela miaka 30, baada ya kupatikana na hatia. Mwingine amefungwa maisha kwa kosa la kumnajisi mtoto mdogo wa kiume" anasema Gama wakati wa maadhimisho hayo.

### TOKOMEZA ZIRO

Mgeni rasmi kwenye maadhimisho hayo, Mkuu wa Wilaya hiyo Jokate, anasema ni kampeni iliyoanzishwa mwaka 2017 ikilenga kuhamasisha na kuinua elimu wilayani Kisarawe.

Anasema mpango huo wenye malengo ya kuongeza ufaulu, kwa wanafunzi wa msingi na sekondari, ulilenga pia kuondoa divisheni ziro na daraja la nne wilayani humo.

Halikadhalika Mkuu wa Wilaya anasema ulilenga kuwapa wasomi muda wa kutosha wa kukaa makambini, kufundishwa zaidi na kujisomea kwa bidii hatua iliyozaa matunda.

Anaongeza kuwa kutokana na operesheni tokomeza ziro wanafunzi wilayani Kisarawe wamefaulu na kwa kuthibitisha jitihada hizo mwaka 2017 zimeanza kuonyesha mafanikio kwa kuinua kiwango cha ufaulu.

Mkuu wa Wilaya Jokate anasema ufaulu umekuwa wa juu mwaka huu na kwamba wanafunzi wa kidato cha nne wamefaulu kwa asilimia zaidi ya 80.

Anaongeza kuwa wilaya hiyo imefanikiwa zaidi na imekuwa na shule nyingi za sekondari zinazotoa elimu ya kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita wakati mwaka 2017 ilikuwa moja sasa ziko tano.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# 300 waliokuwa wasisome wapata neema

## ■ Sekondari, ufundi, ujasiriamali vyote bure

"NINA furaha kila wakati si kwa sababu ya kuwa na kitu kingine chochote, bali ni kuzungukwa na upendo pamoja na kupata bure elimu ya sekondari bora, licha ya kwamba ninatoka kwenye familia maskini mno."

Ni ushuhuda wa Pendo Juma, anayesoma katika Shule ya Sekondari ya Masista wa Maria,iliyoko Makurunge wilayani Kisarawe, wakati wa maadhimisho ya siku ya mtoto wa kike duniani, alipohojiwa na Nipashe, akiwa Kisarawe mkoa wa Pwani.

Binti huyo kutoka kaya maskini mkoani Morogoro anasema yeye na wenzake wengi kutoka familia masikini kupindukia wanapata elimu bora na ujuzi wa kiufundi.

Ni wanufaika wa huduma za kusaidia wahitaji duniani zinazotolewa na watawa wa Kanisa Katoliki wa Shirika la Masista wa Maria.

Shule ya Sekondari ya Masista wa Maria Tanzania, inasomesha mabinti maskini ambao wazazi na walezi wao hawana uwezo wa kuwapa elimu ya sekondari na kuwasaidia kwa lolotea kutokana na umaskini wa familia.

Sekondari hiyo huwapa pia elimu hiyo na ya ufundi bure pamoja na mahitaji yote ya wanafunzi, anasema Pendo.

Anakumbusha kuwa ni mzaliwa wa Morogoro vijijini familia yake inaishi mbali na shule na haina uwezo, kwake ni faraja kubwa kupata nafasi katika shule ya bweni kwa vile vijijini hata kama angepata nafasi huenda angekuwa muathirika wa mimba za utotoni na udhalilishaji.

"Tunajifunza kushona, upishi na ujasiriamali pamoja na elimu ya sekondari vyote ni bure hatugharamii..." anasema na kuwatia moyo wanafunzi wengine akiwaambia wasikate tamaa bali wamuombe Mungu.


Anaungwa mkono na Efrasia Nziku kutoa mkoani Njombe, anayesifu taasisi hiyo kwa kuwapa elimu bora, kuwatoa katika lindi la umaskini ambao hakuna ambaye angewakumbuka.

"Leo tunasoma, tuko karibu na shule hakuna umbali wala manyanyaso dhidi ya mabinti wa familia maskini. Tunafahamu upishi wa vyakula mbalimbali kama keki, mikate, biskuti na tunafahamu kushona mavazi mbalimbali. Tunaujua ujasiriamali. " Anasema Efrasia.

Wasichana hawa wanasomeshwa na watawa kutoka Korea Kusini, wanawaomba Watanzania kuwaunga mkono masista wanaowasaidia ikiwa ni pamoja kuwapa mahitaji yote ya kibinadamu kuanzia chakula, mavazi, malazi na makazi kama kusaidia vifaa vya ujenzi. Akizungumza na Nipashe kwenye maadhimisho ya siku ya mtoto wa kike duniani, ambayo yalifanyika wilayani Kisarawe na kudhaminiwa na vyombo vya habari vya IPP Media, Mkuu wa Shule, Sista Teresa Ladia, anasema wanafanyakazi ya kuhudumia watoto wa familia maskini kupindukia kwa kuwapa elimu bure.

Aidha, anasema wanafundishwa kompyuta na namna mbalimbali za kuzitumia, ujasiriamali, upishi, ufundi wa kushona nguo na kwamba kila kitu wanapata bure.

Anasema mabinti hao wanaosoma bweni wanapewa kila kitu bure, kuanzia mahitaji ya shule, chakula , vifaa na elimu na kwamba wanafundishwa ujasiriamali na ufundi ili kuwawezesha kujitegemea na kuwa na ufahamu mpana zaidi kitaaluma na kiufundi.



Mhashamu Askofu Novatus Rugambwa, mhamasishaji wa kuanzishwa huduma ya kusaidia mabinti fukara nchini. **PICHA: MTANDAO.**

### WANAWAFIKIAJE MASKINI?

Akijibu swali la namna ya kufikia wanafunzi hao wa kaya maskini kupindukia, Mkuu wa Shule anasema wanaosoma wanawasaka kutoka mikoa yote ya Tanzania.

Aidha, ili kuwafikia wanashirikiana na ofisi za wakuu wa wilaya, idara za ustawi wa jamii pamoja na maaskofu wa majimbo mbalimbali kwenye maeneo yanayohusika.

"Wakipatikana tunawachunguza na kuwahakiki, halafu tuwapa mtihani wa kuingia shuleni ili waanze kusoma. Tunasaidia yatima, tuna watoto yatima, wapo wanaolelewa na mzazi mmoja, waliotelekezwa..." anasema."

Mkuu wa Shule anaeleza kuwa wana wasichana 307 ambao wanasoma kuanzia kidato cha kwanza na cha pili na sasa wapo kwenye juhudi zaidi za kuongeza majengo ili kuwa na wanafunzi wengi zaidi.

### WALIFIKAJE TANZANIA?

Sista Ladia anajibu kuwa walifika nchini mwaka 2017 baada ya kuombwa na kukaribishwa Tanzania na Balozi wa Papa nchini Honduras huko Amerika Kusini, Muhashamu Askofu Mkuu Novatus Rugambwa.

Anasema Balozi huyo aliwakaribisha na kuwaomba kuanzisha huduma Tanzania akiwaahidi ushirikiano wake na wa Kanisa pamoja na wadau wa elimu nchini.

Anasema Sekondari ya Masista wa Maria Makurunge ni ya kwanza na ya kipekee barani Afrika na kwamba watawa hao wanafanyakazi ya mataifa ya Korea Kusini, Ufilipini, Guatemala, Brazil, Honduras, Mexico na sasa wako Tanzania.

Akizungumzia historia yao anasema wanafanyakazi kwa kufuata mfano wa mtawa Padri Aloysius Schwartz, wa Marekani aliyeanzisha huduma ya kuwasaidia watoto na jamii maskini kupindukia huko Korea Kusini.

Sista Ladia, anasema Padri huyo, alianzisha Shirika la Masista wa Maria huko 1964 na kwamba tangu wakati huo wamekuwa mstari wa mbele kusaidia wasichana na wavulana maskini kwenye nchi hizo na kwamba kwa Tanzania wameanza na kuwasaidia wasichana.

Anasema licha ya Padri Aloysius Schwartz, kufariki 1992 (alizaliwa 1930) ameacha kazi na jukumu kubwa duniani la kusaidia familia za maskini zisizo na msaada na kwamba wanapewa elimu bora na bure.

Halikadhalika Sista Ladia, anasema walipoingia nchini walijenga shule na kwa kuanza walisomesha wasichana 150, lakini leo wapo mabinti wanufaika 307 wanaosoma kidato cha kwanza na cha pili na kwamba wanalenga kuwaongeza wengine zaidi.

### WASICHANA WANANG'ARA

Akizungumzia mafanikio makubwa yanayoonekana miongoni mwa wasichana kutoka jamii za wahitaji, Sista Asela Ernest anasema watoto hao wanafanya vizuri darasani na kwamba , licha ya kutoka kwenye familia za maskini, wana uelewa mkubwa.

Anasema wanaelewa lugha mbalimbali kwa wepesi, wanafahamu mambo mbalimbali, wanauliza maswali, wana hamu ya kujua mambo na pia ni wajuzi wa kufahamu masuala ya kompyuta na ujasiriamali.

Sista Asela anawasifu kuwa wengi wanajituma na kufanyakazi za ufundi kama upishi na ushonaji kwa weledi na wana nafasi ya kusoma na kuwa watu wenye manufaa makubwa kwa taifa.

Kudhihirisha hilo mabinti hao wakati wa maadhimisho ya siku ya mtoto duniani yaliyofanyika katika Sekondari ya Minaki wilayani Kisarawe , mgeni rasmi akiwa ni Mkuu wa Wilaya Kisarawe, Jokate Mwegelo, waliandaa vitafunwa mbalimbali.

Wanafunzi hao waliandaa keki, biskuti, mikate na maandazi na kuuzia watu mbalimbali ikiwa ni kuonyesha umahiri katika ufundi na pia kufanya kazi za ujasiriamali kwa vitendo.



Sista Teresa Ladia, pamoja na wanafunzi wa Shule ya Masista wa Maria katika maadhimisho ya siku ya binti duniani iliyofanyika Kisarawe Oktoba 11, 2020. **PICHA: GAUDENSIA MNGUMI.**

SAYANSI

NA FAUSTINE FELICIANE

# Faida lukuki za kilimo ikolojia

## •Hakuna sumu, mbolea, GMO

USALAMA wa chakula, maisha endelevu ya viumbe hai na ulinzi wa mazingira ni mambo yanayotatiza dunia zama hizi.

Ni kwa sababu chakula kinalimwa kwa mbolea zenye kemikali na pia huhifadhiwa na dawa zinazoathiri afya na mara nyingi huhusishwa na kuenea kwa maradhi kama saratani na kiharusi.

Lakini wataalamu wanaeleza haja ya kubadilika na kutumia kilimo ikolojia ambao ni ukulima unaochanganya mbinu za asili za kulima kwa lengo la kutunza ardhi kwa kutumia mbolea asilia na viuatilifu visivyo na kemikali kudhibiti wadudu waharibifu.

Aidha, kinaimarisha ardhi iliyochakaa, kinahifadhi unyevu wa udongo hivyo ni muafaka kwenye maeneo yenye ukame. Abdallah Mkindi ni mratibu wa taasisi inayojishughulisha na kilimo cha asili nchini (TABIO), anayesema kilimo ikolojia kinazingatia utunzaji wa anuai za mazao kutoka kwenye mbegu mpaka chakula kinapofika mezani.

Anuai ni mchakato wa utunzaji wa uhai wa asili wa mbegu kuanzia uzalishaji wake hadi kupata chakula.

"Mifumo yetu ya sasa ya kilimo mara nyingi inahimiza ukuzaji wa zao la aina moja. Maeneo makubwa ya ardhi hupandwa mimea inayofanana kinasaba mfano mahindi au mpunga. Njia hii ya kilimo huathiri afya zetu kwa sababu hutupatia milo duni isiyo na virutubisho vya kutosha." Anasema Mkindi.

Anaongeza kuwa kwa kutumia kilimo ikolojia mambo hubadilika kwa kuhamasisha upandaji wa zao zaidi ya moja shambani.

Aidha, kilimo hicho huchanganya teknolojia ya kisasa na maarifa ya wakulima ili kuendeleza aina za mbegu ambazo huongeza uzalishaji na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, bila kuhatarisha viumbe hai wa eneo husika.

Halikadhalika, hakitumii mbegu zilizobadilishwa nasaba wala kemikali za kuulia wadudu.

Mkindi anasema afya endelevu ya udongo na maji safi ni faida nyingine ya kutumia kilimo ikolojia akieleza kuwa inawezekana kuongeza rutuba ya udongo bila ya kutumia mbolea za kemikali. Kilimo ikolojia hulinda udongo dhidi ya mmomonyoko, uchafuzi wa mazingira na ongezeko la tindikali.

"Inawezekana kwa kuongeza matamahuluki (nyasi) ili kuongeza uwezo wa ardhi kuhifadhi maji na kuzuia uharibifu. " anasema Mratibu wa TABIO.

Anataja mbinu nyingine kuwa ni kutumia matamahuluki kwenye udongo, mfano mbolea vunde ambayo ni mabaki ya mimea na samadi kwa kufanya hivyo viumbe vya ardhi hupata chakula.

"Udongo wenye matamahuluki unahifadhi maji nyakati za ukame, usiotishiwa na mmomonyoko wakati wa mafuriko.



Mkulima akiandaa mbolea vunde inayoongeza rutuba ya asili ardhini na chakula cha wadudu wanaorutubisha udongo. **PICHA: TABIO.**

**KULINDA MAJI**

Mkindi anakitaja kilimo hiki kuwa ni mahsusi kwa kulinda vyanzo vya maji ya mito, maziwa na chemchem kutokana na kuepuka matumizi ya mbolea za viwandani na kemikali za sumu kudhibiti wadudu na magugu.

Kwa upande wa visumbufu vya mimea kinawawezesha wakulima kukabiliana na wadudu bila kutumia viuatilifu ghali ambavyo vinaathiri udongo, maji na mazingira, afya za wakulima na walaji.

"Viuatilifu vyenye kemikali sumu ni hatari kwa afya zetu na kwa usalama wa dunia. Kwa bahati mbaya, kilimo kinachohamasishwa cha mashamba makubwa cha zao moja kinategemea kiasi kikubwa cha kemikali za kuulia magugu, kuvu na wadudu ili uzalisha uwe na tija."

Mfumo wa kilimo kinachohamasishwa sasa unawafunga wakulima katika uhusiano wa gharama kubwa na kampuni ambayo huuza kemikali hizo.

**KUJITOSHELEZA CHAKULA**

Mkindi anasema kilimo ikolojia ndicho chanzo muhimu cha uzalishaji wa chakula ambacho ni salama kwa walaji na utunzaji wa mazingira.

Walaji wengi wameelimika kuhusu vyakula ambavyo ni salama kwa afya zao, hivyo kuongeza hitaji la vyakula vilivyokuzwa kwa mbinu za kilimo ekolojia.

"Ni fursa kwa vijana katika kuwekeza katika kilimo ekolojia ili kujiongezea kipato na kuendesha maisha yao."

**TEKNOLOJIA ILIVYO**

Anasema kilimo ikolojia kinajumuisha mifumo mbalimbali ya usimamizi wa mazao na mifugo ambayo inalenga kuongeza mavuno kwa kuzingatia matumizi endelevu ya rasilimali asilia.

Aidha, Mratibu wa TABIO, anasema kinapunguza mahitaji ya pembejeo kutoka nje na pia hulinda rutuba ya udongo, maji na hali ya hewa.

"Hukuza viumbe hai, na hakichafui mazingira kwa pembejeo zenye kemikali za sumu au uhandisi wa vinasaba (GMOs)." Anasema Mkindi.

Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO) kilimo hai kina misingi 10.

Kinaitaja kuwa ni viumbe hai, ubunifu na maarifa shirikishi, kujenga mahusiano, ufanisi, urudufishaji (recycling) , ustahimilivu na ulinzi wa maadili ya kibinadamu na kijamii.

FAO inataja masuala ya utamaduni na mila ya chakula, utawala unaowajibika na uchumi jumuishi pamoja na uimara.

FAO inakieleza kuwa kina faida kubwa kwa mkulima na taifa kwa ujumla kwani ni kilimo salama zaidi. Faida nyingine ni kuwapo na uhuru wa chakula kwa kuzisaidia jamii kuanzia wazalishaji na walaji hudhibiti mnyororo wa chakula kwa upande wa namna chakula kinavyozalishwa na nani anayekizalisha.

Katika maeneo mbalimbali duniani, kampuni kubwa chache hudhibiti sehemu kubwa ya mfumo wa chakula na hivyo kuifanya jamii na hasa vijana kuwa vibarua katika uzalishaji wake.

Kilimo hai kinachukua udhibiti huu na kuuweka katika mikono ya wakulima wadogo hasa vijana ambao huzalisha na kusambaza chakula kwa

walaji, uhuru wa chakula unatambua jukumu la wanawake vijana ambao wamerithi ujuzi na maarifa ya kukusanya na kupanda mbegu kutoka kwa mababu na mabibi zao na hivyo kuchangia katika upatikanaji wa aina mbalimbali za vyakula ambavyo walaji wana uhuru wa kuchagua.

Faida nyingine ya kilimo hiki ni kuwa hunufaisha wakulima na jamii ya vijana vijijini na kuchangia maendeleo vijijini.

"Ushahidi wa kilimo ikolojia kote duniani unaonyesha kwamba kikiungwa mkono na serikali nakuwekewa mikakati madhubuti ni mbinu ya kuwabakiza vijana vijijini badala ya kukimbilia mijini" inasema FAO.

Aidha, inaelezwa faida nyingine ya kilimo ikolijia ni pamoja na uzalishaji rafiki wa chakula na ongezeko la mavuno kwa mkulima na kuboresha maisha na afya za kaya maskini.

Ni lazima pia kuwa na mikakati ya kuongeza mavuno kwa njia endelevu zinazozingatia utunzaji wa mazingira, shirika hilo linashauri.

"Swali muhimu ni wapi na jinsi gani vijana na jamii watazalisha chakula zaidi ambacho ni salama kwa mlaji. Kilimo ikolojia kinaweza kuwa jibu."

Ni kwasababu kinazingatia matumizi endelevu ya rasilimali zinazohitajika kwenye kilimo, ubora wa ardhi, kutunza mazingira na kuepuka matumizi ya mbegu zilizobadilishwa nasaba na kutumia kemikali za viwandani.





# Mavunde aahidi kumaliza kero huduma afya Iyumbu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MGOMBEA Ubunge Jimbo la Dodoma Mjini kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), Anthony Mavunde, amesema endapo akichaguliwa atawaondolea kero ya muda mrefu wananchi wa Iyumbu ya kukosa huduma za afya siku za Jumamosi na Jumapili.

Wananchi hao wamekuwa wakikosa huduma za afya siku hizo kutokana na kutokuwapo kwa nyumba ya daktari wa Zahanati ya Iyumbu.

Akizungumza juzi na wananchi wa Kata ya Iyumbu kwenye mkutano wa kampeni, Mavunde alisema atahakikisha katika miaka mitano ijayo anajenga nyumba ili watumishi wa afya waishi kwenye eneo hilo na kutoa huduma kwa wananchi muda wote.

"Mkinichagua miaka mitano ijayo nitafanya kwa kushirikiana na diwani wenu wa CCM tutajenga nyumba ya daktari ili afanye kazi jumamosi na jumapili tofauti na ilivyo sasa," alisema.

Aliongeza: "Tupeni kura tutaanza kujenga nyumba ya daktari serikali itatukuta mbeleni, sisi tutaanza na ndugu zangu niwaambie mmekuwa mkipata kero kubwa kutokana na Jumamosi na Jumapili hampati huduma kutokana na watumishi hawakai hapa."

**Mwaka 2015 mtakumbuka zahanati hii ilikuwa haitoi huduma stahiki hasa kwa kinamama, nikagharamia ukarabati wa wodi ya akinamama na kuiweka katika hali nzuri sana na kwasasa mnafurahia huduma.**

Aliwashukuru kwa kumchagua miaka mitano iliyopita ambapo walionyesha imani kubwa kwake na kuahidi kuendelea kuwatumikia kwa miaka mitano mingine.

"Mwaka 2015 mtakumbuka zahanati hii ilikuwa haitoi huduma stahiki hasa kwa kinamama, nikagharamia ukarabati wa wodi ya akinamama na kuiweka katika hali nzuri sana na kwasasa mnafurahia huduma,"alisema.

Aidha, aliwaomba wananchi hao kura za Rais John Magufuli ili aendelee kuipasha Tanzania kwa miaka mingine mitano ijayo.

Alibainisha kuwa kwa muda mrefu wananchi wa Iyumbu walikuwa wakihangaika kuhusu fidia ya maeneo yao yaliyochukuliwa kwa ajili ya makaburi ya viongozi wa kitaifa, lakini Rais Magufuli aliwarejeshea eneo hilo lenye hekari 129.

"Mlikuwa mmekata tamaa, nilimuomba Rais na nyie mkiwapo akakubali na amerudisha hekari 129 za wananchi zipo mikononi mwenu," alisema.

Kwa upande wake, mgombea udiwani wa CCM wa Kata ya Iyumbu, Elias Sutuchi, alisema: "Nipeni miaka mitano niibadilishe kata hii ambayo kwa muda mrefu imekuwa chini ya diwani wa upinzani, mimi nilikuwa Mwenyekiti wenu wa Mtaa nazijua shida zenu na kero zenu naahidi kuwatumikia kwa uadilifu na uaminifu mkubwa."

Akimuombea kura Rais Magufuli, Mbunge wa zamani wa Kigoma Kaskazini, Peter Serukamba, alisema Watanzania wana kila sababu kumchagua Magufuli kutokana na kutatua kero zao zitokanazo na umaskini, maradhi na ujinga kwa vitendo.

"Magufuli ameibadilisha Dodoma, amefanya kazi kubwa sana, ameletea heshima Dodoma, Naomba mchague Magufuli na mleteeni na kijana wake Mavunde ambaye amefanya kazi kubwa Dodoma ili kwa umoja wao waendelee kuipaisha Dodoma," alisema.



Watu wenye ulemavu wa kusikia (viziwi), wakimsikiliza mfasiri wa lugha ya alama (mwenye shati jeupe), kwenye mkutano wa kampeni ya uchaguzi uliokuwa wa Chama cha ACT- Wazalendo, wakati mgombea wa udiwani alipokuwa akijinadi kuomba kura kwa wakazi wa Kata ya Majengo, uliofanyika jana jijini Dodoma. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Sababu kuongezeka vituo vya mafuta hizi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa ongezeko la shughuli za kiuchumi na mtandao wa barabara nchini umechangia vituo vya mafuta kuongezeka kwa asilimia 9.32.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Idara ya Petroli wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (EWURA), Gerald Maganga, hadi kufikia Desemba 2019, idadi ya vituo vya mafuta vinavyofanya kazi ilifikia 1,596 kutoka 1,460 kwa mwaka 2018.

Alisema taarifa ya utendaji wa sekta iliyotolewa hivi karibuni na Mamlaka hiyo inaonesha ongezeko hilo ni la asilimia 9.32.

"Kuongezeka kwa vituo hivi kumechangiwa na ongezeko la mahitaji, shughuli za kiuchumi lakini ujenzi wa barabara ambapo vituo vingi vimejengwa maeneo ya kwenye miji, ingawa kuna ongezeko kubwa la mahitaji ya mafuta vijijini," alisema.

Alisema EWURA imeendelea kuhamasisha ujenzi wa vituo vya mafuta vijijini ili kuhakikisha bidhaa hiyo inapatikana kwa uhakika na usalama.

"Kanuni za uuzaji rejareja wa mafuta maeneo ya vijijini za mwaka 2017 zitaendelea kutumika, ambapo baadhi ya mahitaji kwa ajili ya kibali cha ujenzi wa kituo kwa maeneo hayo yamepunguzwa ili kupunguza gharama za uwekezaji bila kuathiri masuala ya afya, usalama na uhifadhi wa mazingira," alisema.

Akizungumzia kuhusu mafuta yaliyoingizwa kwa ajili ya matumizi soko la ndani mwaka 2019, Maganga alisema yalikuwa lita bilioni 3.5 ambapo ni ongezeko la asilimia 8.4 ikilinganishwa na lita bilioni 3.2 za mwaka uliopita.

"Ongezeko hilo lilichangiwa na miradi mingi ya serikali inayoendelea ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara, reli ya kisasa (SGR) na bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere, pia mafuta yanatumika kwenye shughuli za kilimo,"alisema.

Kuhusu gesi ya kupikia, Mkurugenzi huyo alisema biashara hiyo imeendelea kukua kwa kasi ambapo kwa mwaka 2019 jumla ya tani 166,436 ziliingizwa nchini ikilinganishwa na tani 142,939 zilizoingizwa mwaka 2018, hivyo ongezeko ni asilimia 16.

Maganga alisema licha ya ongezeko hilo kuna tatizo la usambazaji usiokidhi mahitaji maeneo ya vijijini na kuwataka wasambazaji wa gesi kupanua mtandao ili kuwafikia wenye kipato cha chini.

# Vijana waonyeshwa fursa kwenye jumuiya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Mwinyi Talib Haji, amewataka vijana kuchangamkia fursa zilizopo kwenye jumuiya mbalimbali ambazo Tanzania ni mwanachama.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akifungua mafunzo ya elimu kwa umma kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Dodoma na Viwandani Sekondari kuhusu kazi na majukumu ya wizara hiyo.

Alisema vijana wanatakiwa kutumia fursa zilizopo kwenye Jumuiya mbalimbali ambazo Tanzania ni mwanachama ili kunufaika na mambo mbalimbali ikiwemo soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Pia, alisema Tanzania ni mwanachama katika jumuiya mbalimbali ikiwamo EAC, pamoja na Jumuiya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Alisema, katika jumuiya hizo zipo fursa mbalimbali ambazo kama vijana wa Kitanzania watajikwamua kiuchumi kutokana na kulitumia soko la pamoja kufanya biashara zao.

"Katika jumuiya hizi ambazo Tanzania ni mwanachama zipo fursa nyingi sana ambazo kama vijana wa kitanzania watazitumia vizuri zitawanufaisha kutokana na kupata fursa ya kufanya biashara zao mbalimbali katika nchini wanachama," alisema Dk. Mwinyi.

Aidha, alisema kuwa Wizara hiyo ina jukumu la kulinda maslahi ya Taifa na kuhakikisha kuwa kama Taifa linanufaika na uwanachama wake katika jumuiya zote.

Vile vile, Naibu Katibu Mkuu huyo alisema kuwa mafunzo hayo yatakuwa endelevu katika shule zote nchini ili kuwajengea uelewa wanafunzi kuhusu kazi na majukumu ya wizara hiyo na fursa zilizopo.

Naye, Mkurugenzi wa Habari wa Wizara hiyo, Emmanuel Buhohela, alisema kuwa lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha vijana kutambua kazi na majukumu ya wizara hiyo.

Alisema vijana wengi wamekuwa hawatambui majukumu ya wizara hiyo pamoja na fursa zilizopo katika jumuiya mbalimbali ambazo Tanzania ni mwanachama hivyo kupitia mafunzo hayo yatawajengea uelewa.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo kutoka Shule ya Sekondari Viwandani, Rahma Husseni, alisema kuwa mafunzo hayo yatamsaidia kuwapatia uelewa mpana juu ya Wizara hiyo pamoja na fursa zilizopo.





# Wizara yaridhishwa na utekelezaji mradi maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WIZARA ya Maji imesema imeridhishwa na utekelezaji wa mradi wa maji wa Shongo ambao unahudumia wakazi wa Mamlaka Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya ambao umekamilika na wananchi wameanza kupata huduma.

Ujenzi wa mradi huo ni utekelezaji wa agizo la Rais Dk. John Magufuli alilolitoa Aprili, mwaka jana alipokuwa ziarani mkoani Mbeya baada ya wananchi wa Mji huo kumweleza kuhusu uwepo wa kero hiyo na akaielekeza Wizara ya Maji kuitatua.

Jopo la maofisa kutoka wizarani walifanya ziara mwishoni mwa wiki kwenye mradi huo wakiongozana na maofisa wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA) pamoja na wa Wakala wa Maji mijini na vijijini (Ruwasa).

Mkuu wa Kitengo cha Tehama wa Wizara ya Maji, Joash Nyitambe, ambaye aliongoza jopo hilo, alisema waliamua kutembelea mradi huo ili kujiridhisha kama kweli umekamilika na unaakisi fedha zilizotolewa na Serikali.

**Lakini pia mradi huu umesaidia kuongezeka kwa ajira maana hawa watu wanaouza maji kwenye vioski (vituo vya kuuzia maji), wameajiriwa na wanapata fedha ambazo zinawasaidia kuendesha maisha.**

Alisema mradi huo ni miongoni mwa miradi muhimu nchini kutokana na kwamba umegharimu fedha nyingi na ulilenga kuhudumia idadi kubwa ya wananchi wa mji huo wa Mbalizi pamoja na vijiji vilivyoko jirani na mradi huo.

"Huu mradi unaridhisha sana, ukiwasikiliza hata wananchi wenyewe wanasema wanaridhishwa na huduma ambayo wanaipata sasa hivi, wanasema hata bei imepungua tofauti na ilivyokuwa mwanzo," alisema Nyitambe.

Aliwataka wananchi wa Mji huo kuendelea kuilinda miundombinu ya miradi mbalimbali ya maji inayowahudumia akidai kuwa kuna baadhi ya maeneo watu wanajihujumu wenyewe kwa kuharibu miundombinu hiyo.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya, Mhandisi Ndele Mengo, alisema kabla ya mradi huo kukamilika, Mji wa Mbalizi ulikuwa ni miongoni mwa maeneo ambayo yalikuwa yanakabiliwa na uhaba wa huduma ya maji.

Alisema wananchi walikuwa wananunua maji kwa gharama ya kati ya Sh. 300 na 500 kwa dumu moja la lita 20 lakini baada ya mradi huo kukamilika maji yanauzwa Sh. 50 kwa dumu hilo.

"Lakini pia mradi huu umesaidia kuongezeka kwa ajira maana hawa watu wanaouza maji kwenye vioski (vituo vya kuuzia maji), wameajiriwa na wanapata fedha ambazo zinawasaidia kuendesha maisha," alisema Mengo.

Alisema kwa sasa kazi wanayoifanya ni kuondoa mabomba ya zamani ambayo wananchi walikuwa wanayatumia na kuweka mapya ili kuondoa tatizo la kupasuka kwa mabomba hayo ya zamani unaosababisha upotevu wa maji.

Baadhi ya wananchi wa Mji wa Mbalizi wanaonufaika na huduma hiyo, walisema kwa sasa hawahangaiki kutafuta huduma hiyo kama ilivyokuwa kabla ya mradi huo.

Mmoja wa wananchi hao, Veronica Wiliadi, alisema walikuwa wanatumia gharama kubwa kutafuta maji pamoja na kununua vyombo vya kutunzia lakini kwa sasa gharama imepungua.

Aliishukuru Serikali kwa kutekeleza mradi huo na kwamba hata maeneo ambayo watu walikuwa wanakataa kuishi wakiogopa ukosefu wa huduma hiyo yameanza kupata wakaazi.



Mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mbeya akimwagilia maua ambayo yamepandwa shuleni hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wakulima wa nyanya wataka sumu ya uhakika

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa nyanya mkoani Mbeya, wamewaomba watafiti wa kilimo kuwatafutia sumu ya uhakika ambayo inaweza kuwadhibiti wadudu wanaoshambulia zao hilo wajulikanao kwa jina la kanitangaze ambao wamekuwa wakiwasababishia hasara.

Wanadai kuwa wadudu hao wamekuwa wakibadili tabia mara kwa mara na hivyo kusababisha udhibiti wake kuwa mgumu wakidai kuwa kwa sasa wameanza kushambulia na mazao mengine yakiwemo mahindi.

Mmoja wa wakulima hao, Majuto Sanga, alisema tangu wadudu hao walipoanza kushambulia nyanya walikuwa wanatumia sumu za aina mbalimbali lakini wadudu hao hawafi.

Alisema kuna baadhi ya wataalamu waliwaambia kuwa ili kukabiliana na wadudu hao inatakiwa kubadili mazao mara kwa mara kwenye mashamba yao lakini wadudu hao nao wamebadilika na kuanza kula mazao mengine ambayo wanapanda.

Alisema kwa muda wa miaka miwili iliyopita wadudu hao wamekuwa wakishambulia mahindi na hivyo kuongeza gharama zingine kwenye uzalishaji wa zao hilo.

"Ukipiga sumu wakati wadudu hao wameshaingia kwenye mazao hawafi, wana njia zao za kujificha na hivyo ukipuliza sumu yoyote hawafi, sasa kilimo hiki kinaanza kutushinda wengi maana sasa hivi wengine wameacha na wengine tumepunguza mashamba," alisema Sanga.

Naye Fabian Mheluke, alisema wadudu hao wanaweza kawasababisha madhara mengine kwa wananchi hasa kutokana na sumu ambazo zinatumika kwenye kilimo hicho.

# Sugu ajivunia heshima anayopewa Mbeya Mjini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Joseph Mbilinyi 'Sugu', amesema hakuna kiwango cha fedha ambacho anaweza akawalipa wananchi wa Jiji hilo kwa heshima wanayompa.

Aliyasema hayo juzi kwenye mkutano wake wa kampeni katika Kata ya Isyesye ambapo alisema tangu alipoingia kwa mara ya kwanza kwenye siasa za kuwania jimbo hilo mwaka 2010 amekuwa akiheshimiwa kwa kiwango kikubwa na wananchi wa Jiji hilo.

Alisema wananchi hao wamekuwa wakihudhuria mikutano yake na hata anapopata tatizo lolote wamekuwa wakishirikiana naye kutatua na hivyo anahisi hakuna aina ya fedha ambayo anaweza akawalipa.

"Sina Dola, Yen, Euro wala Rupia ambazo naweza kuwalipa wananchi wa Mbeya kwa heshima hii mnayonipa, kitu pekee ninachoweza kuwalipa ni kushirikiana nanyi kwenye shughuli za maendeleo," alisema Sugu.

Aliwataka wananchi hao kumpigia kura kwenye uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu ili aendelee kuwatetea kwenye mambo mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanafanya shughuli zao za kujiongezea kipato.

Alisema kabla ya yeye kuwa mbunge wa Jimbo hilo mwaka 2010 lilikuwa linaongozwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho hakikuwasaidia wananchi hao.

Sugu alisema kama mgombea yeyote anayedai kuwa atawaletea maendeleo wananchi hao kwa sasa awaeleze pia kabla ya kuwania nafasi hiyo alikuwa na msaada gani kwao.

Katika hatua nyingine Sugu alisema kuna baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakipotosha baadhi ya vitu ambavyo viongozi wa chama chake wamekuwa wakihoji serikali ikiwemo ununuzi wa ndege kuwa wanapinga vitu hivyo visinunuliwe.

Alisema chama hicho hakijawahi kukataa kununua ndege na ndiyo maana hata wao waliahidi mwaka 2015 kuwa endapo wangeshinda kwenye uchaguzi na wakaunda Serikali wangefufua Shirika la Ndege Tanzania (ATCL).

"Sisi tulichokuwa tunahoji ni gharama za ununuzi wa ndege hizo pamoja na utaratibu uliotumika ambao sisi tulikuwa tunaamini kuwa sio wa kisheria, sasa kuna watu wanakuja wanawaambia eti sisi tunapinga, sio kweli," alisema Sugu.

Alisema chama hicho kikishinda kitahakikisha wananchi wanakuwa na uhuru wa kuhoji vitu mbalimbali ambavyo wanahisi Serikali yao inafanya vibaya ili virekebishwe.

Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Mbeya Mjini, John Mwambigija, aliwaomba wananchi wa Jiji hilo kuwachagua wagombea wa chama hicho kuanzia ngazi ya rais mpaka madiwani.

Alisema kwa sasa wataendelea kuwaelimisha wapiga kura wao namna sahihi ya kupiga kura ili kuhakikisha hakuna kura zinazoharibika ndani ya Jiji hilo na pia kuhakikisha ushindi unapatikana wa chama hicho.





# Waziri awape angalizo wasaidizi wa Mufti Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Khamis Juma Maalim, amewataka maulamaa walioteuliwa kuwa Wajumbe wa Baraza la Ulamaa Zanzibar, kufanya kazi kwa ushirikiano katika misingi ya Kiislamu na kutenda kazi zao kwa haki.

Alitoa kauli hiyo wakati wa uzinduzi wa Baraza la Nne la Ulamaa Zanzibar, akisema mashirikiano na upendo katika utendaji ni jambo la msingi kwenye kutekeleza majukumu yao.

Aliwaambia Ulamaa ni kazi nzito ambayo inahitaji hekma na busara kujadili na kutatua migogoro pamoja na kuleta haki ili kuondoa mafarakano na kupata usuluhishi katika jamii

Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kabi, akitoa nasaha zake, alisema fatwa au haki haitaki papara bali fikra na busara katika kuamua jambo.

"Suala la kutoa fatwa halihitaji hasira kwani kadhia yake utaitoa kama hutazingatia haki", alifahamisha Shekh Kabi .

Aidha aliwataka waulamaa hao kuliombea taifa liweze kuwa na amani na utuluivu hasa katika kipindi hichi cha uchaguzi mkuu .

Katibu wa Mufti Zanzibar, Khalid Ali Mfaume, alisema uwepo wa Baraza la Ulamaa kwa mujibu wa sheria ya Ofisi ya Mufti, kazi yake kubwa ni kumshauri Mufti wa Zanzibar katika masuala mbali mbali yanayofikishwa kwake.

Aidha ni kutoa haki katika kutatua migogoro au usuluhisho na mengine yanayohusiana na Uislamu yanayofikishwa kwake.

Alieleza kuwa Baraza la Ulamaa lina kazi kubwa ya kutoa miongozo mbalimbali kwa misingi ya Uislamu yanayojitokeza katika jamii ili kuweza kusuluhisha na kutoa haki.

# NEC: Hatuna mgombea aliyejitoa mbio za urais

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema haina taarifa wala haijapokea maelezo rasmi ya kuwapo mgombea wa urais wa Muungano, aliyejitoa kushiriki uchaguzi mkuu wiki ijayo.

Akizungumza na wadau wa uchaguzi Visiwani Zanzibar, Kamishna wa NEC, Hasina Omar alisema kutofanya kampeni kwa baadhi ya wagombea wa urais hakuwaondolei sifa ya ugombea kwenye uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika Jumatano ijayo.

NEC imepitisha wagombea 17 kati ya 19 walioomba kuteuliwa nafasi hiyo ambao watapigiwa kura katika uchaguzi mkuu huo.

Alisema vyama vilivyoteuliwa ni pamoja na AAFP, ACT Wazalendo, ADA TADEA, ADC, CCM ,CCK, CHADEMA, CHAUMMA, Chama cha Wananchi CUF, DP, Demokrasia Makini, NRA, NCCR Mageuzi, SAU, UMD na UPDP.

**Kutokana na hali hiyo NEC imepitisha wagombea wote na watakuwamo katika karatasi ya kupigia kura Jumatano ijayo.**

Alibainisha kwamba NEC imeteua wagombea urais na makamu wao kutoka vyama 15 vya siasa ambapo katika uteuzi huo wanawake wawili walijitokeza na kuteuliwa kugombea kiti cha urais wakati watano wanagombea nafasi ya makamu wa urais.

Alisema kutokana na hali hiyo NEC imepitisha wagombea wote na watakuwamo katika karatasi ya kupigia kura Jumatano ijayo.

Alieleza kwamba ni mara ya kwanza kwa Tanzania vyama vingi vya siasa kusimamisha wagombea wa kiti cha urais hali ambayo inaashiria kukua kwa demokrasia.

Mkurugenzi wa NEC, upande wa Zanzibar, Hamidu Mwanga, alisema kwa mujibu wa katiba ya Tanzania ibara ya 74 (6) tume inasimamia na kuratibu uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani.

Hivyo, aliwahakikishia wananchi kuwa NEC itasimamia uchaguzi huo kwa kufuata katiba, sheria na miongozo ili uwe wa uwazi, uhuru na haki.

Akizungumzia utoaji wa matokeo siku ya uchaguzi alisema ni kosa la jinai kwa mgombea kutangaza matokeo na kazi hiyo inafanywa na tume pekee hivyo aliwasisitiza kujiepusha na kosa hilo.

Aliwaomba wananchi kujitokeza kwa wingi wiki ijayo Oktoba 28, kutumia haki yao kikatiba na pale wanapomaliza kupiga kura kurudi nyumbani kusubiri matokeo.



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein (kulia), akikabidhiwa Qasweeda ya Mwaka wa Kiislam 1442 na Mdhamini wa Jumuiya ya Milade Nabii Association Zanzibar Sheikh. Sherali Champsi, wakati wa hafla ya Maadhimisho ya Maulidi ya Kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W), yaliofanyika katika viwanja vya Maisara Suleiman Jijini Zanzibar jana usiku, kushoto kwa Rais ni Naibu Kadhi Mkuu wa Zanzibar, Hassan Othman Ngawi na Rais Mstaafu wa Tanzania, Ali Hassan Mwinyi. **PICHA: IKULU**

# Dk. Mwinyi awaahidi walimu neema nyingi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Walimu Zanzibar (ZATU), kimemtaka mgombea urais wa Zanzibar kupitia CCM endapo atapata ridhaa ya kuwa Rais awajali walimu.

Rais wa ZATU Seif Muhamed Seif, aliyasema hayo wakati akizungumza na mgombea urais Zanzibar kupitia CCM, Dk. Hussein Mwinyi, wakati Dk Mwinyi, alipokutana na walimu ikiwa ni muendelezo wa kampeni zake za kusikiliza makundi mbalimbali.

Alisema ili taifa liwe na wasomi lazima kuwekeza katika sekta ya elimu na kuwajali wanaowafundisha ambao ni muhimu kuzalisha raia na viongozi bora.

Aidha, Seif alisema walimu wamekuwa wakidharauliwa na kuonekana hawana umuhimu kutokana na kutowekewa mazingira mazuri hasa ya kimaslahi.

Rais wa ZATU alimuomba mgombea huyo endapo atakua rais wa Zanzibar aangalie maslahi yao kwa sababu wapo baadhi ya viongozi hawaoni umuhimu wao.

Alieleza kwamba iwapo kungekua na mfumo imara wa kushughulikia matatizo yanayowakumba walimu kusingekuwa na changamoto zinazowakabili walimu nchini.

Aidha alimpongeza Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, kwa kuongeza bajeti ya Wizara ya Elimu hivyo kuendeleza utamaduni huo katika sekta hiyo ambayo ina jukumu kubwa la kuwajenga watoto wa fani na sekta zote.

"Tungejisikia wanyonge kama tusingeonana na wewe kwa sababu umekutana na makundi mbalimbali tumefarajika kukuona na kueleza changamoto zetu na naamini utakapoingia madarakani utatutizama kwa jicho la huruma,"alisema.

Katibu wa chama hicho, Mussa Omar Tafurwa, ameiomba serikali inayokuja kuziangalia upya sheria na sera ya elimu ambazo ni za muda mrefu na haziendani na wakati.

Aidha, aliiomba kufanyiwa marekebisho sheria ya Elimu ya Zanzibar ya mwaka 1982 ambayo imepitwa na wakati licha ya kufanyiwa mapitio 1986 lakini bado haiendani na zama za sasa.

Tafurwa aliomba katika sheria hiyo kuwekwe uhusiano wa dhati kati ya Wizara ya Elimu na Chama cha Walimu Zanzibar na sheria hiyo imlinde mwalimu.

"Kuna baadhi ya walimu walituhumiwa kubaka na wengine kuiba mitihani hivyo kuwepo na sheria ya kumlinda endapo atakuwa hahusiki na tuhuma hizo, "alisema Katibu Mkuu.

Alisema barani Afrika ni Zanzibar pekee haina Tume ya Utumishi ya Walimu hivyo aliomba kuazishwa kwa chombo hicho muhimu.

Akizungumzia maslahi ya walimu alisema ni lazima kushirikishwa katika muundo wa tume ya walimu na kumuomba mgombea huyo akiwa rais kuwalipa walimu asilimia 25 ya mishahara yao posho ya mazingira magumu.

Aidha alisema kilio kingine cha walimu ni kutopandishwa madaraja ya utumishi. Katibu huyo aliomba mafao ya matibabu kwa walimu kutokana na kupanda kwa gharama mbalimbali za maisha.

Kwa upande wake mgombea urais wa Zanzibar kupitia CCM Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema serikali atakayoiongoza itaboresha mazingira kwa walimu wa Zanzibar ikiwamo kuongeza posho kwa walimu wakuu na kuwapandisha madaraja walimu.

Alisema walimu ni watu muhimu katika nchi na hivyo atawapa maslahi bora ili waendelee kuzalisha wataalamu watakaotumika katika nchi yao.

Dokta Mwinyi alisema akipata ridhaa ya kuiongoza Zanzibar atashughulikia suala la nyongeza za posho hizo kutokana na kuwa posho inayotolewa hivi sasa ni ndogo.

"Sioni tatizo kuongeza posho kwa walimu kwa wakuu hawa kama serikali itakuwa na uwezo wa fedha. Kwa mujibu wa taarifa za ZATU inaonyesha kuwa ombi hili lilikuwa limekubalika lakini utekelezaji wake ulikuwa bado kutokana na corona hivyo nitalishughulikia,"alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**DEREVA NA MAUZO**, KATIKA KAMPUNI YA MAJI NAFASI 8 0767 - 269677.

## NYUMBA/VIWANJA NA MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA IKO KAHAMA** MAJENGO VYUMBA VITATU INA MAJI NA UMEME, PLOT No 759, BLOCK "E", KIWANJA NI MEDIUM SIZE. MAWASILIANO ZAIDI; 0759359933/0713553819

**Nyumba self container** ina fence maji na umeme inapangishwa ipo Segerea kwa bibi bei 1,800,000 kwa nusu mwaka 0754467237/0754284708

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA NA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL)** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumaliza tenda etc. Kwa maelezo zaidi piga: **0758 112 332. Karibu EFL**

## OFISI ZA MATANGAZO

**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, RAISSA COMPANY LTD** tutauza kwa mnada wa hadhara gari la mdaiwa Sugu, mali ya Ndugu **NAYAZ NIAZIM BHANJI (T 111 CHF- TOYOTA FORTUNER).** Gari lipo katika yard ya Dalali. Lengo ni kufidia/ kupunguza deni la mkopo analodaiwa. Mnada utafanyika Tarehe 26/10/2020, mahali dhamana ilipo. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi. Raissa Company Ltd: 0652 113 262; Tujijenge: **0718068335/ 0717956315.**

115949902

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**
**Wilaya ya DODOMA**

**MADAI NAMBARI. 63/2020**

**MDAI ANDREA YOHANA SUMBWE**

**MDAIWA UPENDO YOHANA SUMBWE**

**Kwa UPENDO YOHANA SUMBWE**
**IHUMWA- DODOMA**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba TALAKA**

Hivyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya Tarehe 02/11/2020 saa 2.30 asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Na kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama itadhibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakamahii leo tarehe 19/10/2020

115949702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;313/2020**

**Ombi la PETER ALBINO ZAKARIA ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ZAKARIA HARUBINI ALBINO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 19/12/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 19/10/2020.

Sahihi ya Hakimu

115950002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;307/2020**

**Ombi la HENRY SADIKI MLANGE ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu CONSTANSIA PIUS KIHWELE.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 16/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 13/10/2020.

Sahihi ya Hakimu

115950202

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI Na. 75 YA MWAKA 2020**

**MAOMBI YA BARUZA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU SHABANI MUSSA MHANDO**

**MWOMBAJI/WAOMBAJI....ESTHER MSAFIRI MHANDO**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapop juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 30 Mwezi wa Octoba, 2020.
Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 30 Mwezi wa Septemba, 2020.

NAIBU MSAJILI

115950102

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JULIUS JOEL MKALE**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina FUSO yenye namba za usajili **T 897 AGK.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/739574/2020.**

115949602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;311/2020**

**Ombi la REHEMA JUMA MANGO ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu JUMA WAZIRI MANGO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 18/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 15/10/2020.

Sahihi ya Hakimu

115949302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;308/2020**

**Ombi la IDDY AHMED FUKO ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MWAJUMA IDD MADOLLA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 16/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 13/10/2020.

Sahihi ya Hakimu

115949302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84)**

**MAHAKAMA YA MWANZO YA MJINI WILAYA YA MOROGORO**

**MADAI NAMBARI...58..2017**

**Mdai; MARIA SIMON MTWEVE**

**Anamdai**

**Mdaiwa; LUCKAS SANGA**

**Kwa; LUCKAS SANGA**
**MOROGORO**

Kwakuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai Yake/Yao Kwamba/Eleza Hapa habari ya madai; Madai ya Tsh.8,205,000/= Kwahiyo anahitjiwa/Mnahitajiwa katika Mahakama hii siku ya Juma TATU tarehe 26/10/202/ Saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo,na kwakuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta Mashahidi wako/wetu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama hukuudhuria /Hamkuhudhulia siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha Kama umepokea /Mmepokea Kuitwa shaurini hii,Itaweza kutoa hukumu kuwa Umeshindwa/Mmeshindwa.Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 15/10/2020.

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Mjini

115948802

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**IBRAHIM HIMID IBRAHIM**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **LANDROVER** yenye namba za usajili **T.447 BCM** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi **MBE/MBE/RB/44683/2020.**

115949102


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Maelfu waandamana mauaji ya mwalimu

**PARIS,** Ufaransa

MAELFU waandamana nchini Ufaransa kumuunga mkono Samuel Paty, mwalimu aliyekatwa kichwa kwa kuonesha wanafunzi vibonzo vya Mtume Muhammad.

Watu katika eneo la de la République mjini Paris walikuwa wameshika vipeperushi vilivyoandikwa "Je suis enseignant" (Mimi ni mwalimu), wakati waziri mkuu Castex amesema: "Sisi ni Ufaransa!"

Mwanamume mmoja anayeitwa Abdoulakh A, alipigwa risasi na polisi siku ya Ijumaa baada ya kumuua, Paty karibu na maeneo ya shule karibu na mji wa Paris.

Watu 11 wamekamatwa kwa ajili ya uchunguzi ingawa hakuna taarifa zilizotolewa kuhusu kukamatwa kwao.

Ndugu wanne wa karibu wa washukiwa walishikiliwa kwa muda mfupi baada ya mauaji hayo.

Watu wengine sita walishikiliwa siku ya Jumamosi , akiwemo baba wa wanafunzi ambaye alitambulishwa na vyombo vya habari vya Ufaransa kuwa alikuwa muhubiri na muislamu mwenye itikadi kali.

Rais Emmanuel Macron alisema ukatwaji wa kichwa wa mwalimu katika kitongoji kilichopo kaskazini magharibi mwa mji wa Paris -Ufaransa ni "Shambulio la ugaidi wa uislamu" na mwalimu huyo aliuawa kwa sababu alikuwa anafundisha uhuru wa kujieleza.

Mauaji hayo yanakuja baada ya shambulio la mwaka 2015 la Charlie Hebdo ambalo lililengwa na washambuliaji kwa kuchapisha katuni za Mtume Mohammad.

Eneo la de la République mjini Paris lilijaa watu wengi wakimuunga mkono bwana Paty, 47. Bwana Castex na Paris Mayor Anne Hidalgo walijumuika nao.

Makutano hayo yalijaa watu wengi wapatao milioni 1.5 wakionyesha mshikamano kwa Charlie Hebdo kufuatia shambulio kubwa lililotokea Januari 2015.

Muandamanaji mmoja siku ya Jumapili alikuwa amebeba bango lenye maelezo "Maadui wote wa Jamhuri hawawezi kuvumilika kabisa" na mwingine alisema "Mimi ni profesa. Ninakufikiria wewe, Samuel."

Mwingine alisema Le Figaro alikuwa muislamu wa Ufaransa alieelezea machungu ya mauaji hayo.

Dakika moja ya ukimya huko Marseillaise. Waandamanaji wote walikuwa wamevalia barakoa kujikinga na virusi vya corona.

Waziri wa elimu Jean-Michel Blanquer alisema Ufaransa itafanikiwa kukabiliana na maadui wake wa demokrasia kama wataungana kwa pamoja na kwa walimu wote wa Ufaransa wanahitaji kuungwa mkono.

Nathalie, mwalimu kutoka Chelles alikuwa katika maandamano ya Paris , Le Monde ilisema alikuwa hapo kwa sababu aligundua kuwa unaweza kufa kwa kufundisha tu. **BBC**

# Kenya hatarini wimbi jipya janga la Corona

**NAIROBI,** Kenya

WAZIRI wa Afya wa Kenya, Mutahi Kagwe, amesema maofisa wa afya wanafuatilia mwenendo wa wanasiasa wanaokiuka maagizo ya kisayansi na kufanya mikutano ya kisiasa yenye mikusanyiko ya watu wengi.

**Wagonjwa 10 wanapumua kwa usaidizi wa machine, huku 14 wakiwa wameekewa oxygen. Kati ya wagonjwa ambao wamelazwa hospitalini, 50 ni raia wa kigeni.**

Waziri ameonya kwamba nchi hiyo ipo katika hatari kubwa ya kutokea wimbi jipya la maambukizi ya virusi vya corona, kwa sababu wanasiasa wanaendelea kukaidi maagizo ya maofisa wa afya, huku kiwango cha maambukizi kikiendelea kuongezeka.

Akihutubia waandishi wa habari, Kagwe, alisema kwamba kiwango cha maambukizi ya virusi vya corona kimeongezeka nchini humo, akiripoti visa vipya 685 jumapili pekee.

Alionya uwezekano wa "kutokea janga kubwa la kiafya" akieleza kwamba vijana wanaendelea "kupuuza hatari ya virusi hatari vya Corona."

Kagwe, alisema kwamba maofisa wa afya wanaendelea kufuatilia mwenendo wa wanasiasa wanaokiuka maagizo ya kisayansi na kufanya mikutano ya kisiasa yenye mikusanyiko ya watu, akionya kwamba huenda hatua kali zikalazimika kutumika kurejesha nidhamu kati ya raia.

Waziri huyo wa afya alieleza kwa masikitiko kwamba "watu walio omba sana shughuli za kawaida zifunguliwe, ndio wanaoongoza katika kukiuka maagizo ya kudhibiti maambukizi ya virusi vya Corona".

Kulingana na Wizara hiyo, kiwango cha maambukizi nchini humo kimefikia asilimia 12 kutoka asilimia 4 wakati serikali ilipolegeza masharti ya kupambana na virusi hivyo na kuruhusu raia kurejea hali yao ya maisha ilivyokuwa awali lakini kwa tahadhari.

Kufikia Oktoba 18, mwaka huu, watu 28 walilazwa katika chumba cha kuwahudumia wagonjwa mahtuti baada ya kuambukizwa virusi vya Corona, huku idadi ya jumla ya wagonjwa kutokana na virusi hivyo ikiwa imefikia watu 1,000.

Kaimu mkurugenzi wa huduma za afya nchini Kenya Patrick Amoth, alisema idadi ya wagongwa wanaolazwa hospitalini imeongezeka kutoka 450 hadi 991 katika mda wa siku moja.

Wagonjwa 10 wanapumua kwa usaidizi wa machine, huku 14 wakiwa wameekewa oxygen.

Kati ya wagonjwa ambao wamelazwa hospitalini, 50 ni raia wa kigeni.

Mji wa Nairobi unaongoza kwa maambukizi, ukifuatiwa na Nakuru, Mombasa, Trans Nzoia, Kisii, Kiambu, Kakamega, Kisumu, Busia, Kilisi na Nandi. **VOA**



Raia wa Guinea wakiwa katika foleni ya kupiga kura katika uchaguzi wa urais, Oktoba 18, mwaka huu, eneo la Fria, Guinea. Hadi jana kura zilikuwa zinaendelea kuhesabiwa huku Rais Alpha Conde aliyepo madarakani akiwania muhula wa tatu. **PICHA: REUTERS**

# Rais Conde akaribia ushindi Guinea

**CONAKRY,** Guinea

RAIS wa sasa nchini Guinea, Alpha Conde (82), anatarajiwa kuibuka mshindi huku kura zikiendelea kuhesabiwa, baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika mwishoni mwa wiki.

Conde, iwapo atashinda itakuwa muhula wa tatu madarakani.

Aidha, nchini Ivory Coast, watu wawili wamefariki katika ghasia za uchaguzi mkuu, unaotarajiwa kufanyika wiki mbili zijazo kwenye nchi hiyo ya Afrika Magharibi.

Polisi wameimarisha usalama kote nchini Guinea baada ya kutokea ghasia katika sehemu tofauti za nchi, kupinga hatua ya Conde kuwania muhula wa tatu.

Polisi walisema kwamba shughuli ya kupiga kura ilifanyika katika mazingira yenye utulivu.

Uchaguzi huo umefanyika baada ya miezi kadhaa ya maandamano yaliyopelekea watu kadhaa kuuawa katika msako wa maofisa wa usalama dhidi ya waandamanaji waliokuwa wakimpinga rais Alpha Conde.

Conde anakabiliwa na ushindani mkali kutoka kwa kiongozi wa upinzani Cello Diallo na wagombea wengine 10.

Tayari Diallo amedai kwamba huenda rais Conde akafanya udangayifu katika kuhesabu ya kura.



Kumekuwepo wasiwasi kwamba machafuko ya hivi karibuni yamechukua mkondo wa kikabila, rais Conde akishutumiwa kwa kusababisha migawanyiko kwa manufaa yake ya kisiasa, shutuma ambazo amekana.

Siasa za Guinea hugubikwa sana na ukabila. Rais Conde anatoka jamii ya Malinke huku mpinzani wake - Diallo, akitoka jamii ya Fulani.

Kuna wasiwasi mkubwa nchini Guinea kwamba huenda kukatokea ghasia baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi ambayo yatachukua muda kutolewa. **VOA**




# TRAORE KUZIKATA MAINI LIVER, BARCELONA

**LONDON,** England

ADAMA Traore ameripotiwa anajiandaa kusaini mkataba mpya wa kuendelea kubaki hapo Wolves wakati klabu za Barcelona na Liverpool zikiwania saini yake.

Traore amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka pale Wolves, ambapo alitua mwaka 2018 akitokea Middlesbrough.

Lakini winga huyo anaonekana kuwa na furaha zaidi kucheza kwenye Ligi Kuu ya England na hivyo hana mpango wa kuondoka.

Traore sasa anatarajiwa kuongezewa mshahara na atasaini mkataba wa miaka minne kuendelea kuwachezea Wolves akizitosa ofa za Barcelona na Liverpool, kwa mujibu wa gazeti la The Sun.

Nyota huyo ambaye ameichezea Hispania mechi tatu za kimataifa mkataba huo mpya utamfanya acheze hapo hadi mwaka 2023.

Barcelona na Liverpool kwa muda mrefu sasa zimekuwa zikihaha kukimbizana kuwania saini ya Traore.

# Aston Villa yajiwekea rekodi yake EPL

**LONDON,** England

KOCHA Dean Smith amesifia ushindi wa Aston Villa wakati wakiwa kwenye kiwango bora cha kihistoria kwa mwanzo bora zaidi wa Ligi Kuu msimu huu.

Villa ilibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Leicester City, Jumapili shukrani kwa bao la dakika ya mwisho kupitia kwa Ross Barkley na kuwafanya washinde mechi nne kati ya nne kwenye Ligi Kuu.

Smith ambaye kikosi chake hicho cha Villa kilikaribia kushuka daraja msimu uliopita kimeshinda mechi nne za ufunguzi wa Ligi Kuu kwa mara ya kwanza, tangu msimu wa 1930-31.

"Niliwaambia wachezaji mwanzoni mwa msimu lazima kutengeneza historia," alisema kocha huyo wa Villa ambaye timu yake sasa inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi nyuma ya Everton.

"Tulifanya hivyo msimu wangu wa kwanza kwa kushinda mechi 10 na tukabahatika kubaki Ligi Kuu msimu uliopita. Na sasa tunatakiwa kuendelea kuweka rekodi ya kushinda kila mchezo.

"Haya ni matokeo makubwa kwa sababu tumemfunga kocha mkubwa, Brendan Rodgers na timu yake.

"Msimu uliopita walikuwa kwenye nne bora na ni moja ya timu ngumu, hivyo lazima tujisikie fahari kwa rekodi yetu.






# *Guardiola amwonya Aguero mkataba mpya*

**MANCHESTER,** England

SERGIO Aguero lazima athibitishe kama anaweza kupewa mkataba mpya pale Manchester City, Pep Guardiola ameonya.

Aguero alirudi uwanjani kwa mara ya kwanza baada ya kukosekana kwa miezi minne kutokana na kuumia goti wakati City wakipata ushindi wa bao 1-0 nyumbani dhidi ya Arsenal kwenye Ligi Kuu ya England, Jumapili.

Lakini mshambuliaji huyo ambaye anaongoza kwenye orodha ya wafungaji wa wakati wote wa City, mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu na Guardiola amesema Aguero ana nafasi ya kuthibitisha kwamba anapaswa kupewa mkataba mpya.

"Sergio sasa anatakiwa kuonyesha, kama ilivyo kwa kila mmoja wetu, kwamba anastahili kuendelea kuwapo hapa kuendelea kucheza vizuri, kufunga mabao na baada ya hapo klabu na mimi tutaamua," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Lakini kama akicheza kwa kiwango chake hatutakuwa na shaka naye kwani ni aina ya wachezaji tunaowataka wabaki kikosini mwetu. Kwani ni mchezaji muhimu kwetu, kwa mashabiki na kwa kila mmoja.

"Lakini alikuwa nje kwa miezi minne na anatakiwa kujifua kila siku na kuanza kufunga mabao zaidi hiki ni kitu muhimu zaidi kwake."

Aguero ameshinda mataji manne ya Ligi Kuu tangu atue hapo City akitokea Atletico Madrid mwaka 2011.

## HABARI MICHEZO

# Mourinho: Kwenye soka mambo hayo hutokea

**LONDON,** England

JOSE Mourinho alikuwa na wakati mgumu kuelezea namna walivyoanguka wakati wanaongoza kwa mabao matatu na mwishowe kujikuta wakiondoka na pointi moja baada ya kutoka sare.

Tottenham ilikuwa inaongoza kwa mabao 3-0 hadi dakika ya 81 dhidi ya West Ham, lakini mambo yalibadilika ghafla na kujikuta wakimaliza mchezo huo wa Ligi Kuu England kwa sare ya mabao 3-3.

Na Mourinho mara baada ya mchezo huo wa Jumapili alisema: "Kwenye soka mambo hayo hutokea".

Spurs walianza mchezo huo kwa bao la dakika ya 14 la Son Heung-min na Harry Kane akafunga mara mbili.


Wakati wenyeji wakionekana kuelekea kupata ushindi, katika dakika ya 82, Fabian Balbuena aliifungia West Ham na hapo ndio mambo yalipobadilika kabisa kwa kikosi hicho cha David Moyes.


Haraka Davinson Sanchez akajifunga kabla ya Manuel Lanzini kufunga bao la kusawazisha dakika ya mwisho katika mchezo huo na kupata sare hiyo.

Bao la Lanzini liliifanya West Ham kuwa timu ya kwanza kwenye historia ya Ligi Kuu ya England kuepuka kipigo baada ya kuwa nyuma kwa mabao matatu hadi dakika ya 81.

Alipoulizwa kwenye mahojiano na Sky Sports baada ya mchezo huo ili aelezee kilichotokea, Mourinho alijibu: "Ni mpira wa miguu."

"Bila shaka siwezi kuzungumza sana, nimeangalia kipindi cha pili, mambo yalibadilika, lakini huwa inatokea kwenye soka."





# CAVANI TAYARI KUIVAA PSG LEO

**MANCHESTER,** England

EDINSON Cavani alianza mazoezi na Manchester United kwa mara ya kwanza Jumapili baada ya kumaliza kipindi cha kukaa karantini alikokuwa amejitenga.

Cavani alijiunga na United katika siku ya mwisho ya kufungwa kwa pazia la usajili kama mchezaji huru kutoka Paris Saint-Germain.

Hata hivyo, kutokana na sheria za serikali ya Uingereza kwa mlipuko wa virusi vya corona zinawataka watu wote wanaoingia nchini humo kujitenga kwa siku 14.

Raia huyo wa Uruguay aliingia nchini humo akitokea nchini Ufaransa ambapo ni moja ya nchi ambayo watu wake wanapaswa kujitenga wakiingia Uingereza, hivyo akalazimika kukaa karantini kwa siku 14.

Cavani hakuweza kucheza mchezo wa Ligi Kuu wa Jumapili dhidi ya Newcastle United, maana yake sasa anaweza kuanza kwenye mchezo wa leo Jumanne wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya timu yake ya zamani, PSG.

Wakati wakijiandaa kwenda nchini Ufaransa kwa ajili ya mchezo huo, United ilichapisha picha kwenye mitandao yake ya kijamii Jumapili kuonyesha nyota huyo mwenye umri wa miaka 33, akiwa ameanza mazoezi na wachezaji wenzake.

Cavani alikaa miaka saba kule Parc des Princes, akifunga mabao 200 kwa muda wote aliokuwa kwenye klabu hiyo ya Ligue 1.

# Welbeck ajiunga na Brighton

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United na Arsenal, Danny Welbeck, amejiunga na Brighton and Hove Albion.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, ambaye aliondoka Watford mwishoni mwa msimu uliopita, amesaini mkataba wa mwaka mmoja na kikosi hicho cha kocha Graham Potter.

Anaweza kuanza kuichezea timu hiyo kwenye mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya West Brom Oktoba 26, mwaka huu.

"Tunafuraha kuwa na Danny aliyejiunga kwetu. Ataimarisha safu yetu ya ushambuliaji," alisema Potter kupitia tovuti ya Brighton.

"Ana kiwango kisicho na shaka kabisa, ni mchezaji mzuri na mwenye kasi ya kucheza vizuri safu ya ushambuliaji.

"Atatuongezea mbinu kwenye safu yetu ya ushambuliaji kwa sababu ni mchezaji mwenye uzoefu na ubora."

Welbeck alianza kwenye mechi tisa tu za ligi kwa misimu miwili iliyopita, akiwa amekabiliwa zaidi na majeraha ya mara kwa mara miaka ya hivi karibuni.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VAN DIJK ATOA NENO 'AKIPIGWA' KISU GOTINI

●●● Nitarudi nikiwa bora, fiti na imara, kwa sasa akili yangu ni kuhakikisha napona haraka...

**LUVERPOOL,** England

NYOTA wa Liverpool, Virgil van Dijk, ameahidi kurudi akiwa "bora, fiti na imara" baada ya kufanyiwa upasuaji wa goti.

**Mabingwa wa Ligi Kuu ya England, Liverpool walithibitisha Jumapili kwamba mlinzi wao huyo aliumia goti na atafanyiwa upasuaji na hivyo atakosekana kwenye sehemu kubwa ya msimu huu.**

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi alitarajiwa kufanyiwa upasuaji huo baada ya kuumia wakati wa mchezo wa timu za jiji moja, Everton na Liverpool uliomalizika kwa sare ya mabao 2-2 kabla ya yeye kugongana na golikipa, Jordan Pickford na kuumia goti hilo.

Katika taarifa aliyoichapisha kwenye ukurasa wake wa Twitter, Van Dijk alisema anashukuru kwa sapoti aliyoipata wakati akijiandaa kufanyiwa upasuaji.

"Mchana huu (juzi) nilikutana na watalaamu wa afya kwa ajili ya kuanza utaratibu wa kufanyiwa upasuaji baada ya tukio lililotokea Jumamosi," aliandika. "Kwa sasa akili yangu ni kuhakikisha napona haraka na nitafanya kila kitu kuhakikisha narudi uwanjani haraka inavyowezekana.

"Licha ya yote imani yangu inaniambia pale penye magumu Mungu hufanya wepesi na kwa uwezo wake nitahakikisha narudi nikiwa bora, fiti na imara zaidi kuliko mwanzo.

"Katika soka, kama ilivyo maisha ya kawaida, naamini kila kitu huwa kinatokea kwa sababu ni muhimu kuzingatia kile kilichotokea kwa mtazamo chanya.

"Kwa sapoti ya mke wangu, watoto, familia yangu na kila mmoja hapa Liverpool, nipo tayari kwa changamoto mpya iliyopo mbele yangu.

"Ningependa kumshuruku kila mmoja aliyenitumia ujumbe wa kuonyesha sapoti, ina maana kubwa sana kwangu mimi na familia yangu, na nitafanya kila niwezalo kuwapa sapoti wachezaji wenzangu.

"Kuna wiki zinakuja za mechi ngumu nitakuwa nyuma ya wachezaji wenzangu kila siku wakati nikiwa kwenye harakati za kupambana ili nipone mapema. Nitarudi tu."

Vijana hao wa Jurgen Klopp wapo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi wakiwa na pointi 10 baada ya mechi tano za ufunguzi wa wakipitwa pointi tatu na Everton.

## ZISIKUPITE

### MATUMAINI KWA SANCHO

MANCHESTER United imepewa tumaini kwamba inaweza kumsajili winga wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 20, baada ya "kumhukumu vibaya" waliposhindwa kumpata msimu uliopita. ***(Star)***

### KANTE HAONDOKI CHELSEA

KIUNGO wa Ufaransa, N'Golo Kante mwenye umri wa miaka 29, hana mpango wa kuondoka Chelsea muda wowote licha ya kuwaniwa na Real Madrid na Inter Milan. ***(Star)***

### ROONEY KWENYE CORONA

KOCHA mchezaji wa Derby County, Wayne Rooney mwenye umri wa miaka 34, jana Jumatatu alitarajiwa kupewa matokeo ya vipimo vya corona, baada ya kugundua kuwa rafiki yake aliyemuuzia saa ya mkononi alikuwa na virusi hivyo. ***(Daily Telegraph)***

### ATAKA LIVER ISAJILI

MLINZI wa zamani wa Liverpool, Jamie Carragher, amesema klabu hiyo lazima itafute beki wa kati kwenye dirisa la usajili la Januari baada ya kuumia kwa Virgil van Dijk mwenye umri wa miaka 29. ***(Mail)***

### ATOBOA SIRI BLACKBURN

WINGA wa Liverpool, Harvey Elliott, mwenye umri wa miaka 17, alikitathmini kwanza kikosi cha Blackburn kabla ya kukubali kujiunga na timu hiyo. ***(Mail)***

### GOMES AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United pia wanamlenga kiungo wa kati wa Sporting Lisbon mwenye umri wa miaka 16, Luis Gomes. Kiungo huyo raia wa Ureno amepewa jina la utani la 'Luis Figo' ajaye nchini humo. ***(Mirror)***

### TRAORE KUJIFUNGA ZAIDI

WINGA wa Wolves, Adama Traore mwenye umri wa miaka 24, yuko tayari kusaini mkataba mpya na klabu hiyo, licha ya kuwaniwa na Barcelona na Liverpool. Mkataba huo mpya utamfanya alipwe mshahara wa pauni 100,000 kwa kwenye dimba la Molineux. ***(Mail)***

### DYBALA, OFISA WAZOZANA

MSHAMBULIAJI wa Juventus na Argentina, Paulo Dybala, mwenye umri wa miaka 26, alikuwa na malumbano na Ofisa Mkuu wa Soka wa klabu hiyo, Fabio Paratici baada ya kuachwa nje ya kikosi cha Jumamosi. ***(Mail via Tuttosport)***

### WIJNALDUM KUTUA BARCA

KIUNGO wa kati wa Liverpool na Uholanzi, Georginio Wijnaldum, anaweza kujiunga na Barcelona wakati wa dirisha la usajili la Januari. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, kwa sasa yuko mwaka wa mwisho wa mkataba wake na msimu ujao atakuwa huru. ***(AD, via Sky Sports)***

### MAN CITY YAIGOMEA BARCA

MANCHESTER City imekataa ofa ya dau la pauni milioni 15.4 na marupurupu kutoka kwa Klabu ya Barcelona ili kumnunua beki, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 19, katika siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la uhamisho. ***(Sky Sports)***

# SVEN AHOFU SOKA LA NGUVU LA PRISONS LITAITESA SIMBA

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kikosi cha wachezaji 22 cha Simba kikitua salama jijini Mbeya jana tayari kwa kambi ya siku mbili kabla ya kuifuata Tanzania Prisons mjini Sumbawanga, Kocha Mkuu wa mabingwa watetezi hao, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, ametabiri mchezo mgumu kutokana na wapinzani wao kucheza soka la kutumia nguvu zaidi.

Simba imejichimbia jijini Mbeya kuanzia jana na leo kabla ya kesho kuanza safari ya kuelekea Sumbawanga tayari kwa mechi yao ya Ligi Kuu dhidi ya Tanzania Prisons itakayopigwa Alhamisi katika Uwanja wa Nelson Mandela.

Akizungumzia mchezo huo, Sven alisema anategemea utakuwa mgumu kutokana na Prisons kucheza soka lenye matumizi makubwa ya nguvu, lakini amejipanga kukabiliana nao kuhakikisha wanapata pointi tatu.

**Sven alisema ameondoka na wachezaji 22 ambao anaamini wanatosha kwa ajili ya mchezo huo na wote wako vizuri kiafya tayari kuipigania timu yao hapo keshokutwa.**

"Mechi dhidi ya Prisons tunaamini itakuwa ngumu kama zilivyo nyingine za ugenini, kwa sababu ni timu inayocheza soka la matumizi makubwa ya nguvu, lakini tumejiandaa kuwakabili.

"Hatujaondoka na kikosi kizima, tumesafiri na wachezaji 22 tu kwa ajili mechi hii, tuna matumaini makubwa ya kufanya vizuri na tutahakikisha tunalifanikisha hilo," alisema Sven ambaye kikosi chake kipo katika nafasi ya pili ya msimamo wa ligi hiyo kabla ya mechi za jana.

Simba yenye pointi 13, tano nyuma ya Azam FC iliyopo mbele mchezo mmoja, itaivaa Prisons yenye alama tano kabla ya mechi yao ya jana dhidi ya JKT Tanzania iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Lakini pia Simba itashuka katika Uwanja wa Nelson Mandela, ikiwa na kumbukumbu nzuri ya kupata matokeo uwanjani hapo kutokana na ushindi wa mabao 2-0 waliyoyapata kwenye mechi ya fainali ya Kombe la FA dhidi ya Namungo FC Julai mwaka huu.



Kiungo wa Simba, Mghana Bernard Morrison, akishusha mizigo yake kwenye ndege baada ya mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara kwa miaka mitatu mfululizo, kuwasili jijini Mbeya jana kwa kambi ya siku mbili kabla ya kuelekea mjini Sumbawanga mkoani Rukwa tayari kwa mchezo wao wa ligi hiyo dhidi ya Tanzania Prisons utakaopigwa keshokutwa, Alhamisi katika Uwanja wa Nelson Mandela. **PICHA: SIMBA**

# Ihefu yamtoa Katwila mechi ya Azam

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Ihefu FC, imesema haitomhukumu kocha wake mpya, Zuberi Katwila, kwa matokeo yoyote yale ambayo timu hiyo itayapata leo itakapocheza dhidi ya Azam FC kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Zagalo Chalamila, alisema kocha huyo ndiyo kwanza amejiunga na kikosi hicho, hivyo anahitaji muda wa kukinoa taratibu ili kutengeneza falsafa na mfumo wake.

"Tumefanya maboresho makubwa kwenye kikosi chetu kuhakikisha timu inaimarika na kupata matokeo. Na ndiyo maana tumemchukua Katwila na si yeye tu tutafanya maboresho makubwa, ila muda bado tutatangaza.

"Kuhusu mechi dhidi ya Azam, bado ni mapema sana kwake, hatuwezi kumhukumu kocha kwa mechi hii kwa sababu ndiyo kwanza amejiunga," alisema Chalamila.

Katwila, alitangaza kubwaga manyanga ghafla juzi kuifundisha Mtibwa Sugar ya Turiani Morogoro ambayo bado inasuasua kwenye mechi ya Ligi Kuu na muda mfupi baadaye kutangazwa kuwa Kocha Mkuu wa Ihefu FC ya Mbarali mkoani Mbeya ambayo nayo pia iko hoi kwenye ligi.

"Nimejiunga na Ihefu kwa sababu nimetoka Mtibwa, nilipotangaza kuondoka tu, Ihefu walinifuata nikawasikiliza, nikawakubalia. Mimi ni mwalimu nikaona haina shida nikakubali," alisema Katwila, mchezaji na nahodha wa zamani wa timu hiyo ya Mtibwa Sugar.

Hata hivyo, ameishukuru timu yake hiyo ya zamani kuwa imemfanyia mambo mengi makubwa, lakini amesema amewaelekeza vitu vya kufanya ili timu iendelee hata kama yeye hayupo.

Katwila ni mmoja wa wachezaji walioipa ubingwa wa Tanzania Bara Mtibwa Sugar mwaka 2000 na 2001.

Wakati Ihefu ikiwa na kibarua dhidi ya vinara Azam FC leo, Mwadui FC itacheza dhidi ya waburuza mkia wa ligi hiyo, Mbeya City kwenye Uwanja wa Mwadui Complex, huku Kagera Sugar ikiwa nyumbani katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba kucheza dhidi ya Dodoma Jiji, na Ruvu Shooting itakuwa nyumbani dhidi ya KMC FC.

## TFF yageukia soka la wanawake Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wallace Karia, amesema ili kupiga hatua katika soka la wanawake, ni lazima wapatikane viongozi wengi wanawake, hatua ambayo itasaidia kufikiwa lengo kusudiwa.

Karia alitoa kauli hiyo jana wakati akifungua mafunzo ya siku tano ya uongozi wa soka la wanawake visiwani Zanzibar. Alisema mfumo wenyewe wa mpira wa wanawake hauna budi kuwa nav wengi wanawake ili kuendana na mazingira pamoja na kuwajengea imani wazazi ambao wanawaruhusu watoto wao wa kike kucheza soka.

Alisema elimu inahitajika kutolewa zaidi kwa viongozi hao jambo ambao litasaidia kuendana na kasi ya sasa ya uongozi katika mpira wa miguu nchini.

Alisema katika soka la wanawake, bado kuna changamoto mbalimbali ambazo zimeanza kufanyiwa kazi ikiwamo uchache wa viongozi wa wanawake katika ngazi mbalimbali, waamuzi wanawake na makamisaa, hivyo endapo elimu itatolewa anaamini malengo hayo yatafikiwa.

Awali akimkaribisha mgeni rasmi, Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Seif Kombo Pandu, aliipongeza TFF kwa kufanya mafunzo hayo Zanzibar kwani elimu itakayotolewa itasaidia kuleta mabadiliko kwa washiriki katika mikoa yao.

## Simba Queens walia kuporwa Warundi wao

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba Queens, umesema umeamua kuachana na wachezaji wao wawili raia wa Burundi, Joelle Bukuru na Asha Djafar, ambao wamezuia kurejea Tanzania na Klabu ya PVP FC ya nchini humo, kwa madai kuwa walisajiliwa kinyume cha taratibu.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mratibu wa Simba Queens, Seleman Erassy, alisema waliwasajili nyota hao misimu miwili wakiwa wachezaji huru na kuichezea klabu yao kwa kipindi chote, hivyo wanashangaa uamuzi huo wa PVP FC.

Alisema baada ya kufanya mawasiliano na uongozi wa PVP FC bila ya mafanikio, wameamua kuachana na nyota hao, lakini wataandika barua Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuhitaji msaada wao kwa kukiandikia barua Chama cha Soka Burundi kutafuta suluhu ya tatizo hilo.

"Tumejitahidi kufanya mawasiliano na viongozi wa klabu hiyo, wameonekana kutokuwa tayari kuwaachia, hata hivyo wameshacheza mechi mbili wakiwa na kikosi hicho wakati wakiwa ndani ya mkataba na Simba.

"Hao wachezaji walikuja tukawasajili wakiwa wachezaji huru, suala ambalo tunajiuliza wamecheza misimu miwili Simba, viongozi hao walikuwa wapi? Hivyo kama wanaendelea kuwang'ang'ania basi tumeachana nao na tunahitaji kurudishiwa pesa zetu," alisema Erassy.

Michezo

Jumanne Oktoba 20, 2020

Nipashe



Van Dijk atoa neno 'akipigwa' kisu gotini UKURASA 22

SAMAGOL...



Mshambuliaji wa kimataifa Tanzania na Klabu ya wa Fenerbahce ya Uturuki, Mbwana Samatta (kulia), akimtoka beki wa kimataifa wa Bosnia na Herzegovina anaichezea Goztepe SC, katika mchezo wa Ligi Kuu ya Uturuki uliyopigwa usiku wa kuamkia jana katika Uwanja wa Goztepe Gursel Aksel jijini Izmir. Fenerbahce ilishinda 3-2, shukrani kwa wafungaji, Jose Ernesto Sosa kwa penalti dakika ya 26, Serdar Aziz dakika ya 43 na Dimitris Pelkas dakika ya 51, wakati ya Goztepe SC yote yalifungwa na Guilherme kwa penalti pia dakika ya 34 na lingine dakika ya 63. Ushindi huo uliifanya Fenerbahce kufikisha pointi 11 na kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo. **PICHA: MTANDAO**

## Al Ahly, Zamalek dabi Cairo CAF?

**Na Mwandishi Wetu**

USHINDI wa bao 1-0 iliyoupata Zamalek ya Misri katika mechi ya kwanza ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ugenini juzi dhidi ya mabingwa wa Ligi Kuu ya Morocco, Raja Casablanca, sasa unafanya Dabi ya Cairo ('The Cairo Derby') dhidi ya wapinzani wao wakubwa nchini Misri, Al Ahly kunukia, lakini wakati huu zikitarajiwa kukutana kwenye fainali ya Ligi Mabingwa Afrika.

Jumamosi wapinzani wakubwa wa Zamalek, Al Ahly nao walitanguliza mguu mmoja katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya ushindi wa mabao 2-0 ugenini dhidi ya Wydad Casablanca katika mechi ya nusu fainali iliyopigwa Uwanja wa Mohamed V jijini Casablanca, Morocco.

Shukrani zikiwaendea wafungaji wa mabao hayo, Mohamed Magdi Afsha dakika ya nne na Ali Maaloul dakika ya 62 kwa penalti .

Lakini usiku wa kuamkia jana, Zamalek nayo ikiwa katika uwanja huo huo wa Mohamed V nchini Morocco, iliwazamisha Raja Casablanca kwa bao hilo pekee lililopatikana kupitia kwa Mmorocco mwenzao, Achraf Bencharki anayeichezea klabu hiyo ya Misri.

Nyota huyo wa zamani wa Wydad Casablanca, alifunga bao hilo pekee dakika ya 18 akimalizia pasi ya Ahmed Sayed 'Zizo', hivyo timu hizo mbili za Misri, Al Ahly na Zamalek sasa zinahitaji sare ya aina yoyote ama ushindi katika mechi za marudiano zitakazopigwa Jumamosi na Jumapili ili kutinga fainali.

# KAZE AYAONA MABAO YA YACOUBA, SARPONG

**Na Faustine Feliciane**

### ●●● Aeleza sababu kushindwa kucheka na nyavu, sasa aweka mkazo mambo matatu Yanga, huku...

HUKU akiweka mkazo katika maeneo matatu muhimu, Kocha Mkuu wa Yanga, Mrundi Cedric Kaze, ameeleza yalipo mabao ya washambuliaji wake Michael Sarpong na Sogne Yacouba ambao wanaongoza safu ya ushambuliaji ya timu hiyo.

**Hadi sasa Sarpong amefunga bao moja tu, alilolipata katika mechi ya ufunguzi dhidi ya Tanzania Prisons wakati Yanga ikilazimishwa sare ya bao 1-1, wakati hali ikiwa hivyo pia kwa Yacouba ambaye naye ameziona nyavu mara moja wakishinda 3-0 dhidi ya Coastal Union, mechi zote zikipigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.**

Hali hiyo imekuwa ikizua hofu kwa mashabiki wa klabu hiyo kuhusu ubutu wa makali yao, lakini Kaze amewatetea Sarpong na Yacouba, akieleza kwanza ni wachezaji wapya ndani ya kikosi hicho huku akiwatoa hofu Wanayanga kwa kueleza kuwa ni washambuliaji wazuri wasubiri wataona moto wao.

"Sikiliza, Sarpong na Yacouba wote ni washambuliaji wazuri na wanalijua goli vizuri, aliyependekeza wasajiliwe ni mimi baada ya kuwafuatilia muda mrefu.

"Kinachowasumbua ni kukosa mbinu pamoja na viungo wa kuwatengenezea pasi za kufunga, hicho ndicho kimesababisha hayo yote kutokea. Naamini nitawabadilisha kila kitu na ubora wao utaonekana," alisema Kaze.

Na wakati huu Kaze akikiandaa kikosi hicho kuelekea mechi yao ya keshokutwa, Alhamisi dhidi ya Polisi Tanzania, ameweka msisitizo katika maeneo matatu ambapo ameonekana kugeukia zaidi stamina, kasi na umiliki wa mpira huku akieleza kutarajia kuona mabadiliko hayo kuanzia mchezo huo ujao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaze aliyewasili nchini Oktoba 15, alisema pamoja na kwamba muda aliokaa na wachezaji hao ni mchache, lakini anatarajia mabadiliko makubwa kwenye mchezo wa keshokutwa.

"Kama nilivyosema awali, yapo mambo ambayo nitayatilia mkazo kwa ajili ya mabadiliko ya timu, ndio hayo nimeanza nayo, nitaendelea nayo mpaka pale kutakapoonekana mabadiliko," alisema.

Alisema anafahamu upinzani mkali uliopo baina ya timu yake na mahasimu wao, Simba ambao wanatarajia kuumana nao Novemba 7, mwaka huu, lakini yeye haifundishi timu kwa ajili ya mechi moja.

"Tuna wiki tatu kama sikosei kabla ya mchezo huo, lakini kwangu mimi Yanga siifundishi kwa ajili ya mchezo huo tu, naandaa timu icheze soka zuri la kasi na lenye matokeo chanya kwa michezo yote ya mbele yetu na jambo hilo linawezekana kabisa," alisema kocha huyo ambaye mchezo dhidi ya Polisi Tanzania utakuwa wa kwanza kwake kuiongoza Yanga.

Alisema anafurahishwa na wachezaji wake kwa namna walivyowaelewa kwenye mazoezi anayowapa jambo ambalo linampa faraja ya kufikia malengo yake.

Kaze ataanza kuiongoza Yanga yenye pointi 13 kutokana na kushinda michezo yake minne na kutoka sare mchezo mmoja katika mitano iliyocheza hadi sasa, na baada ya mechi hiyo wataifuata KMC FC katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Lakini kibarua kigumu kwa Kaze kitakuwa dhidi ya watani zao, Simba katika mechi ya ligi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Novemba 7, mwaka huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >